

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, MHESHIWA
DKT. JOHN POMBE MAGUFULI (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA FEDHA KWA MWAKA
WA FEDHA 2015/16**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa fedha 2014/15. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuiongoza Wizara ya Ujenzi ambayo inatoa mchango mkubwa wa maendeleo ya Taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu vyema katika kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Nne (2005– 2015). Weledi na umakini wa uongozi wake hususan katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005–2010 na 2010–2015 umeiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo hususan katika sekta ya ujenzi na hivyo kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Mhe. Rais atabaki katika kumbukumbu za watanzania kwa mchango wake uliotukuka katika kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara, madaraja na vivuko ambavyo ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika taifa letu. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali katika Awamu ya Nne.

4. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyevititi wa Bunge kwa hekima, umahiri na busara mnazotumia katika kuliongoza Bunge hili Tukufu. Pongezi za dhiti pia ziwaendee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu

kwa michango, ushauri na ushirikiano waliotupa katika kuimarisha utendaji wa Wizara. Ushauri na miongozo inayotolewa na Kamati hii imekuwa na manufaa makubwa na tunaizingatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

5. **Mheshimiwa Spika**, mwaka huu wa 2015 Bunge lako Tukufu lilipata simanzi kutokana na kifo cha Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Natoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na kwa familia za marehemu, wananchi wa Mbinga Magharibi na Watanzania wote kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu aendeleo kuipa familia iliyopoteza mpendwa wao moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati nimpungeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, (Mb) kwa hotuba yake inayobainisha mafanikio katika mwaka wa fedha 2014/15 na mwelekeo wa jumla wa mipango ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba hiyo nikiamini kuwa maoni yao yatasaidia kuboresha utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo katika nchi yetu.

Dira na Dhima ya Wizara

7. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Wizara ya Ujenzi ni kuwa na Barabara, Madaraja, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zenye ubora wa kiwango cha juu, zenye gharama nafuu na zinazozingatia usalama na utunzaji wa mazingira. Aidha, dhima ya Wizara ni kuwa na Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji kwa viwango bora na kwa bei nafuu zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na wakati huo huo zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

Majukumu ya Wizara

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi ina majukumu ya kusimamia Sera za Ujenzi na Usalama Barabarani; ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali pamoja na masuala ya ufundi na umeme. Aidha, Wizara inasimamia shughuli za usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; masuala ya usalama barabarani na mazingira katika sekta ya ujenzi; uboreshaji wa utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Wizara

pamoja na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wakala/Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Malengo ya Wizara

9. *Mheshimiwa Spika*, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imelenga kujenga barabara ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu ya mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka wa fedha 2017/18; kuendeleza na kuboresha barabara zinazounganisha mikoa, wilaya na vijiji; Ujenzi wa madaraja, barabara za juu (flyovers) na kuboresha makutano ya barabara katika majiji na miji mikuu hususan jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari; kufanya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa; kujenga barabara za kupunguza msongamano wa magari mijini hususan katika Jiji la Dar es Salaam; kuhakikisha kuwa usafiri wa vivuko unaimarishwa katika maeneo yote yanayohitaji huduma hiyo na kusimamia ujenzi wa nyumba za Serikali na watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kusajili na kusimamia Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa kutumia bodi husika pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Ujenzi. Wizara pia itaendelea kusimamia masuala ya usalama na mazingira katika barabara na vivuko pamoja na kufanya matengenezo na ukarabati wa

magari ya Serikali na mitambo. Vile vile Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi husika katika kushughulikia masuala mtambuka kama vile kampeni za kupunguza maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI, uhifadhi wa mazingira, masuala ya jinsia pamoja na uendelezaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Mikakati ya Wizara katika Kufikia Malengo

10. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuweza kutekeleza malengo yake, Wizara itaendelea kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia mwaka wa fedha 2011/12 – 2015/16, Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Aidha, Wizara ya Ujenzi inazingatia Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu ya Usafirishaji (*Transport Sector Investment Programme – TSIP*) ambayo ni programu ya miaka kumi (2006/07-2016/17) inayolenga kuimarisha na kuboresha miundombinu ya usafirishaji. Wizara itaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003), Sera ya Usalama Barabarani (2009) na Sera ya Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*). Wizara pia itaendelea kusimamia utoaji elimu kwa

wananchi kuhusu matumizi ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 pamoja na sheria nyingine ili miundombinu ya barabara iweze kutunzwa na kudumu kwa muda uliokusudiwa. Wizara vile vile itaendelea kuboresha mfumo wa upimaji magari ya mizigo kwa kuweka mizani itakayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (*Weigh-in-Motion - WIM*) kwa lengo la kupunguza msongamano na ucheleweshaji katika vituo vya mizani.

11. ***Mheshimiwa Spika***, mikakati mingine ni pamoja na kusimamia fedha za Mfuko wa Barabara ili kazi za matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko zinazotekelezwa zilingane na thamani ya fedha iliyotumika (*Value for Money*). Wizara pia itaendelea kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kupanua wigo wa Mfuko wa Barabara. Aidha, Wizara itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria na kanuni za kisekta ili ziweze kuendana na mazingira ya sasa na kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa na kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community - EAC*) na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Development Community - SADC*). Wizara itahakikisha kuwa Makandarasi, Wahandisi Washauri, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa kizalendo wanajengewa uwezo na wanahusishwa kikamilifu katika ujenzi wa

miradi mikubwa hususan miradi ya barabara, madaraja, nyumba na vivuko inayogharamiwa na Serikali badala ya kutegemea kampuni za nje. Lengo ni kuwajengea wazalendo uzoefu stahili katika Sekta ya Ujenzi na kupunguza kasi na wingi wa fedha zinazotokana na vyanzo vyetu kuhamishiwa nje ya nchi kwa kulipia kazi zinazofanywa na kampuni za nje.

B. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KATIKA KIPINDI CHA 2005 – 2015

12. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15, naomba nitoe taarifa ya jumla ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne iliyoingia madarakani mwaka 2005.

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho ni Chama Tawala kuanzia mwaka 2005 hadi 2015. Malengo ya Ilani kwa Wizara ya Ujenzi ni pamoja na kuimarisha Mfuko wa Barabara, ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja, ununuzi/ujenzi wa vivuko na ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali. Wizara imetekeleza majukumu hayo kwa mafanikio makubwa kupitia Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara

14. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne kuanzia mwaka 2005 hadi 2015, Serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **13,753** zimekuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **4,691** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **2,358** zimeendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **3,419** zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na Serikali inatafuta fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye jumla ya kilometa **3,285** unaendelea.

15. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi na ukarabati wa madaraja, jumla ya **madaraja makubwa 30** yapo katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Kati ya hayo, **madaraja makubwa 12** yamekamilika kujengwa, ambayo ni Rusumo (Kagera), Umoja (Mtwara), Mwanhuzi (Simiyu), Kikwete (Kigoma), Nangoo (Mtwara), Ruhekei (Ruvuma), Mbutu (Tabora), Mwatisi (Morogoro), Ruvu (Pwani), Nanganga (Mtwara), Maligisu (Mwanza) na daraja la waenda kwa miguu la Mabatini (Mwanza). Aidha, **madaraja makubwa**

6 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambayo ni Kigamboni (Dsm), Kilombero (Morogoro), Kavuu (Katavi), Sibiti (Singida), Ruvu Chini (Pwani) na Lukuledi II (Mtwara). **Madaraja makubwa 12** yako kwenye maandalizi ya kujengwa ambayo ni Momba (Rukwa/Mbeya border), Mwiti (Mtwara), Simiyu (Mwanza), Wami (Pwani), Ruhuhu (Ruvuma), Ubungo Interchange (Dar es Salaam), TAZARA Flover (Dar es Salaam), Selander (Dar es Salaam), Daraja jipya la Wami Chini (Pwani), Pangani (Tanga), Kirumi (Mara) na daraja la waenda kwa miguu la Furahisha (Mwanza). Sambamba na ujenzi wa madaraja makubwa, **madaraja madogo madogo zaidi ya 7,200** yamejengwa na kukamilika.

16. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015 Serikali pia imeimarisha Mfuko wa Barabara ambapo mapato ya Mfuko yameongezeka kutoka Shilingi bilioni **73.08** katika mwaka wa fedha 2005/06 hadi Shilingi bilioni **751.7** katika mwaka wa fedha 2014/15 ikiwa ni ongezeko la asilimia **928.6**.

17. **Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani mwaka 2005, vivuko vya Serikali vilivyokuwa vinatoa huduma vilikuwa kumi na tano (**15**) tu. Hadi kufikia Aprili, 2015, idadi ya vivuko vya Serikali vinavyotoa huduma katika maeneo mbalimbali

nchini imeongezeka na kufikia ishirini na nane **(28)**.

18. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa nyumba na majengo ya Serikali, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo Tanzania ilijenga nyumba **173** za makazi ya Viongozi wa Umma na kuanza mradi wa ujenzi wa nyumba **10,000** za Watumishi wa Umma ambapo nyumba **643** zilikamilika katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015 na nyumba **270** zinaendelea kujengwa. Aidha, Wizara kupitia TBA imeendelea kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba na majengo yanayotumiwa na umma unazingatia mahitaji maalum hususan kwa wenye ulemavu. Suala hili limeendelea kutekelezwa kupitia miradi ya ujenzi wa majengo yote ya Serikali ambayo Wakala wa Majengo umesanifu na kusimamia. Majengo yaliyozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ni kama yafuatayo: Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Manyara, majengo ya ofisi za wilaya za Bariadi, Rorya, Kilolo, Nyamagana na Mvomero. Mengine ni jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi – Kitengo cha Wakimbizi, jengo la hospitali ya Manyara na ukumbi wa mikutano na Vituo vya Afya ya Msingi (Primary Health Centre Institutions – PHCI) – Iringa, majengo ya ofisi ya wakuu wa mikoa ya Katavi, Njombe, Geita na Simiyu pamoja na majengo ya ofisi ya wakuu wa wilaya 19 za Buhigwe, Busega,

Butiama, Chemba, Gairo, Ikungi, Itilima, Kalambo, Kaliua, Kakonko, Kyerwa, Mbogwe, Mkalama, Mlele, Momba, Nyang`hwale, Nyasa, Uvinza na Wanging'ombe.

C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2014/15

Ukusanyaji wa Mapato

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 41,123,000.00 kupitia Idara zenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Utawala, Huduma za Ufundi na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi. Hadi kufikia Aprili, 2015, jumla ya Shilingi 40,750,000.00 zilikuwa zimekusanywa.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha Shilingi 557,178,792,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 24,338,319,000.00 ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi, Shilingi 6,640,073,000.00 ni Matumizi Mengineyo na Shilingi 526,200,400,000.00 ni fedha za Mfuko

wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Hadi kufikia Aprili, 2015 Shilingi 225,090,856,696.00 zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, Shilingi 22,668,779,629.00 zimetolewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na Shilingi 2,723,177,067.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Wizara ya Ujenzi imepokea fedha za Mfuko wa Barabara kutoka HAZINA jumla ya Shilingi 199,698,900,000.00 ambapo Shilingi 34,346,900,000.00 ni za mwaka wa fedha 2013/14 na Shilingi 165,352,000,000.00 ni za mwaka wa fedha 2014/15.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

21. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliidhinishiwa na Bunge Shilingi 662,234,027,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni Shilingi 450,000,000,000.00 na Shilingi 212,234,027,000.00 zilikuwa fedha za nje. Fedha zilizotolewa hadi Aprili, 2015 ni Shilingi 444,729,086,445.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi

250,000,000,000.00 ni fedha za ndani na Shilingi 194,729,086,445.00 ni fedha za nje.

Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Madaraja

22. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) inasimamia mtandao wa barabara kuu na za mikoa wenye urefu wa kilometa 35,000. Katika katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ilipanga kufanya matengenezo ya kawaida na muda maalum (routine and periodic maintenance) ya barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa kilomita 31,132.22, matengenezo ya muda maalum kilomita 4,450.27 matengenezo ya sehemu korofi kilometa 1,075.61 na madaraja 2,802.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara unaendelea vizuri. Kwa upande wa barabara kuu, jumla ya kilomita **504.4** kati ya kilomita **539** zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami zilikuwa zimekamili hadi kufikia Aprili, 2015. Aidha, kilomita **87.75** kati ya kilomita **165** zilizopangwa kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami zilikamilika. Kwa upande wa barabara za mikoa, kilomita **40.5** kati ya

kilomita **94** zilizengwa kwa kiwango cha lami. Vile vile, kilomita **450** kati ya kilomita **1,350** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe katika kipindi hicho.

24. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Madaraja ya Mbutu na Maligisu ulikamilika katika mwaka 2014/15. Aidha, ujenzi wa madaraja makubwa sita (**6**) unaendelea, ambayo ni Kigamboni, Ruvu Chini, Lukuledi II, Kavuu, Kilombero na Sibiti. Vilevile, usanifu wa daraja la Ruhuhu umekamilika.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, jumla ya kilomita **11,453.7** na madaraja **1,364** ya barabara kuu yalipangwa kufanyiwa matengenezo. Aidha, kilomita **25,284.2** na madaraja **1,440** ya barabara za mikoa yalipangwa kufanyiwa matengenezo. Hadi kufikia Aprili, 2015, matengenezo yaliyofanyika katika barabara kuu ni jumla ya kilomita **5,968.5** na madaraja **772** na kwa upande wa barabara za mikoa matengenezo yaliyofanyika ni jumla ya kilomita **8,111.2** na madaraja **537**.

26. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari katika mwaka wa fedha 2014/15 kwa kutumia mizani 36 ya kudumu na 22 inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi Aprili, 2015, magari yapatayo 2,594,485 yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo 676,006

yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya fedha iliyokusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida ilikuwa ni Shilingi 4,021,413,995.00.

27. **Mheshimiwa Spika**, barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200)** sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100) imepangwa kujengwa kwa kiwango cha “Expressway”. Maandalizi ya mradi huu utakaotekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP) yameanza. Hadi kufikia Aprili, 2015, Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor) ambaye ni Kampuni ya *Cheil Engineering Company Limited* kutoka Korea ya Kusini amekamilisha utafiti wa mwelekeo wa barabara (route survey). Mwelekeo wa barabara uliochaguliwa unaanzia Charambe katika barabara ya Kilwa kupitia Kisarawe, Kibamba, Kibaha, Mlandizi hadi Chalinze. Barabara hii yenye urefu wa kilometa 128 itakuwa ya njia sita (6) na barabara za juu (interchange) tano (5) katika maeneo ya Charambe, Kisarawe, Kibamba, Mlandizi na Chalinze. Aidha, kutakuwa na vituo vikuu viwili (2) vya kulipia tozo ya barabara (Toll Plaza) maeneo ya Charambe na Chalinze. Pia barabara hii itakuwa na eneo la kupumzika (rest station) pale Visiga na maeneo mawili (2) ya kugesha malori

ambayo yatakuwa Mbezi na Mbala. Vilevile Mshauri Mwelekezi atafanya utafiti wa jinsi ya kuunganisha barabara hii kutoka Charambe hadi bandari ya Dar es Salaam. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi anaendelea na kazi ya kuandaa nyaraka za zabuni na baadaye atasimamia taratibu za kumpata Mbia/Mwekezaji (Concessionaire) wa mradi huu.

28. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu ujenzi wa **Daraja Jipya la Selander** ambalo lengo kuu ni kupunguza msongamano wa magari katika eneo la Selander, Serikali ya Korea Kusini imekubali kuipatia Serikali ya Tanzania mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa Daraja jipya la Selander. Upembuzi yakinifu wa mradi huu umekamilika na maandalizi ya kutiliana saini ya makubaliano ya mkopo wa kugharamia ujenzi wa wa daraja kati ya Korea Exim Bank (kwa niaba ya Serikali ya Korea Kusini) na Serikali ya Tanzania yanaendelea. Daraja hili pamoja na barabara zake za maingilio litakuwa na urefu wa jumla ya kilometa 7.2 na litaanzia eneo la Koko Beach kupitia barabara ya Kenyatta Drive na kuingia baharini kuungana na barabara ya Barack Obama eneo la Hospitali ya Aghakan.

29. ***Mheshimiwa Spika***, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa **barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Makofia – Msata (km 108)** kwa

sehemu ya Bagamoyo – Msata (km 64) zinaendelea. Hadi kufikia Aprili, 2015 Mkandarasi amekamilisha tabaka la lami km 59.2 na kazi za ujenzi wa madaraja likiwemo daraja la Ruvu Chini zimekamilika kwa asilimia 70.

30. ***Mheshimiwa Spika***, barabara ya **Bagamoyo – Saadani – Tanga** yenye urefu wa kilometa 178 inahusisha kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ya usanifu wa kina wa barabara hii ilikuwa imekamilika.

31. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa** yenye urefu wa kilometa 422 umegawanywa katika awamu tatu kama ifuatavyo: Kyamyorwa hadi Geita (km 220), Geita hadi Usagara (km 90) na Uyovu hadi Biharamulo (km 112). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

Kyamyorwa – Buzirayombo (km 120)

Kazi za ujenzi wa km 120 zilikamilika Februari 2008. Kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu kiliisha Agosti, 2011. Hata hivyo kutokana na

mashimo kujitokeza mapema katika baadhi ya maeneo katika mradi huo kipindi cha uangalizi kiliongezwa hadi Agosti, 2012. Hadi sasa Mkandarasi anaendelea na kazi za matengenezo ya sehemu ya barabara iliyoharibika yenye urefu wa km 41 kwa gharama zake mwenyewe.

Buzirayombo – Geita (km 100)

Ujenzi wa barabara hii ulikamilika Februari, 2008 na kipindi cha uangalizi kimekamilika Machi, 2011. Barabara hii imepokelewa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Usagara – Geita (km 90) (Lot 1 na Lot 2)

Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Geita – Sengerema (km 50) na Sengerema – Usagara (km 40). Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Geita – Sengerema (km 50) zilikamilika mwezi Januari, 2010 na kipindi cha uangalizi (Defects Liability Period) cha miaka mitatu (3) kilikamilika Januari, 2013. Mradi umepokelewa na TANROADS tarehe 12 Aprili, 2013. Ujenzi wa sehemu ya Sengerema – Usagara (km 40) ulikamilika tarehe 7 Agosti, 2010. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15, zilikuwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Uyovu – Biharamulo (km 112)

Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili (2) na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

Uyovu – Bwanga (km 45)

Hadi Aprili, 2015 Mkandarasi alikuwa anaendelea na kazi ambapo madaraja yote yamekamilika. Kazi zingine zilizokamilika ni kusafisha barabara (clearing and grubbing) km 45, ujenzi wa tuta km 26.5, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 21 na tabaka la msingi (base course) km 6.7.

Bwanga – Biharamulo (km 67)

Hadi kufikia Aprili, 2015 Mkandarasi alikuwa anaendelea na kazi za ujenzi na amekamilisha kazi zifuatazo: kusafisha barabara (clearing and grubbing) km 52, ujenzi wa tuta km 27, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 11.5 ambapo makalavati makubwa (box culverts) 20 na madogo (pipe culverts) 25 yamekamilika.

32. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 504.7)** kwa kiwango cha lami ni kama ifuatavyo: –

Tabora – Ndono – Urambo (km 94)

Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili ambazo ni Tabora – Ndono (km 42) na Ndono – Urambo (km 52). Hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: –

Tabora – Ndono (km 42)

Ujenzi wa mradi huu ulikamilika tarehe 6 Februari, 2014 na kipindi cha uangalizi kiliisha tarehe 15 Februari 2015.

Ndono – Urambo (km 52)

Utekelezaji wa mradi huu umefikia hatua zifuatazo: ujenzi wa tuta la barabara km 51, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 47, tabaka la msingi (base course) km 40 na tabaka la lami km 39.

Daraja la Kikwete katika mto Malagarasi na Barabara zake (km 48)

Lengo la mradi huu ni kujenga daraja katika mto Malagarasi na barabara za kuingilia kila upande wa daraja. Mradi huu umetekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza

ilihusisha ujenzi wa daraja na makalavati pamoja na barabara yenye urefu wa kilometa 11. Awamu ya pili ilihusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 37 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi (Economic Development Cooperation Fund) wa Korea Kusini.

Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Awamu ya Kwanza

Kazi ya ujenzi wa daraja na barabara yenye urefu wa kilometa 11 ilikamilika Novemba, 2013 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kilikamilika Novemba, 2014.

Awamu ya Pili (km 37)

Kazi za ujenzi wa kilometa 37 kwa kiwango cha lami zilikamilika Agosti, 2014 na mradi huu uko katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

Uvinza – Kidahwe (km 76.6)

Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umegharamiwa na Mfuko wa Abu Dhabi (Abu Dhabi Fund) pamoja na Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi ilikamilika Oktoba, 2013 na

kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kilimalizika Oktoba, 2014. Fedha zilizotengwa zilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi.

Uvinza – Malagarasi (km 51.1)

Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Uvinza – Malagarasi kwa kiwango cha lami. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Mfuko wa Abu Dhabi (Abu Dhabi Fund) umeahidi kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa sehemu ya barabara hii. Serikali inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizo kutoka ABUDHABI.

Kaliua – Kazilambwa (km 56)

Ujenzi wa barabara ya Kaliua hadi Kazilambwa (km 56) kwa kiwango cha lami ni sehemu ya barabara ya Kaliua – Malagarasi – Ilunde (km 156). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia Aprili, 2015, kazi zifuatazo zimekamilika: ujenzi wa tuta km 18, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 15, tabaka la msingi (base course) km 15, tabaka la lami km 14.6, makalavati makubwa manane (8) na makalavati madogo 17.

Kazilambwa – Chagu (km 40)

Mradi unahusisha ujenzi wa barabara ya Chagu – Kazilambwa yenye urefu wa kilometa 40 kwa

kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi za usanifu wa kina zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Urambo – Kaliua (km 33)

Mradi unahusisha ujenzi wa barabara ya Urambo – Kaliua yenye urefu wa kilometa 33 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi za usanifu wa kina zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Tabora – Sikonge (km 70)

Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tabora – Sikonge sehemu ya Tabora – Usesula (km 30) umesainiwa. Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi.

33. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang’ombe – Sanya Juu** (km 173), ujenzi umegawanywa katika sehemu zifuatazo:

Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32)

Mradi wa ujenzi wa barabara hii umekamilika.

Tarakea – Rombo Mkuu (km 32)

Mradi wa ujenzi wa barabara hii umekamilika.

Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32)

Mradi wa ujenzi wa barabara hii ulikamilika Machi, 2013 na kipindi cha uangalizi kilimalizika Machi, 2014.

Bomang’ombe – Sanya Juu – Kamwanga (km 100)

Lengo la mradi huu ni kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Bomang’ombe – Sanya Juu – Kamwanga (km 100). Hadi kufikia Aprili, 2015 taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya Sanya Juu – Alerai (km 32.2) zimekamilika na mkataba unatarajiwa kusainiwa wakati wowote.

34. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa barabara ya **Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha Bypass (km 140)**, lengo la mradi huu ni kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami kwa njia nne barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta-Voi kwa kuanzia na sehemu ya Sakina –Tengeru (km 14.1) na sehemu ya Arusha Bypass (km 42.4) kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika

(AfDB). Mkataba wa ujenzi umesainiwa Machi, 2015 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi.

35. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa **KIA – Mererani (km 26)** ni kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Mkataba wa ujenzi wa awali ulisitishwa Februari, 2014 kutokana na Mkandarasi kukiuka matakwa ya mkataba. Mkataba mpya wa ujenzi umesainiwa Februari, 2015 na maandalizi ya ujenzi yanaendelea.

36. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa **Kwa Sadala – Masama (km 12.5)** ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 kilometa 9.5 za tabaka la lami zimekamilika na ujenzi wa km 3 zilizobaki unaendelea.

37. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa barabara ya **Nangurukuru – Mbwemkuru** yenye urefu wa kilometa 95 lilikuwa ni kujenga kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (*Design & Build*). Ujenzi wa barabara hii ulikamilika mwaka 2008. Hata hivyo Wizara ya Ujenzi ilikataa kupokea mradi huu kwa kuwa haukukamilika kwa kiwango kilichokusudiwa na hivyo kuwepo kwa marekebisho yaliyohitajika kufanywa na Mkandarsi kwa gharama zake mwenyewe. Kazi ya marekebisho imekamilika

sasa na barabara imepokelewa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

38. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Dodoma – Manyoni** yenye urefu wa kilometa 127, lengo la mradi huu lilikuwa ni kujenga kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa *Design & Build*. Mradi huu ulikamilika Novemba, 2009. Aidha, mradi huu unahusisha kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (km 4.8) ambapo, ujenzi wa km 2.8 kwa kiwango cha lami umekamilika. Kazi za ujenzi wa kilometa 2 zilizobaki unaendelea.

39. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Mbwemkuru – Mingoyo** yenye urefu wa kilometa 95 lengo lake lilikuwa ni kujenga kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (*Design & Build*). Ujenzi wa mradi huu ulikamilika Desemba, 2007 na kipindi cha uangalizi wa mradi cha miaka 3 kilimalizika Desemba, 2010.

40. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Nelson Mandela** yenye urefu wa kilometa 15.6 ulihusu uimarishaji wa barabara na kuboresha mfumo wa mifereji pamoja na taa za barabarani na zile za kuongozea magari. Aidha, mizani ya kupimia uzito wa magari iliwekwa nje ya lango la kutokea bandarini ili kudhibiti uzito

wa magari ya mizigo yanayotoka bandarini. Mradi huu umegharamiwa kwa msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania ulikamilika Juni, 2011. Kipindi cha uangalizi wa mradi cha mwaka mmoja kimeisha mwezi Juni, 2012. Fedha zilizokuwa zimetengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mkandarasi ambayo ni mchango wa Serikali uliopangwa kugharamia mradi huu.

41. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Dumila – Kilosa** yenye urefu wa kilometa 63, lengo ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili ili kurahisisha utekelezaji; sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45) na sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 18). Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Dumila – Rudewa (km 45)

Kazi za ujenzi zimekamilika Desemba, 2013 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kimemalizika Desemba, 2014. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Rudewa – Kilosa (km 18)

Usanifu umekamilika. Ujenzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami unasubiri upatikanaji wa fedha.

42. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Sumbawanga –Matai–Kasanga Port** yenye urefu wa kilometa 112, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design & Build). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia Aprili, 2015, Mkandarasi alikuwa anaendelea na ujenzi ambapo kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo: Usanifu wa kina km 100, kusafisha barabara km 80, tuta la barabara km 65, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 59, tabaka la msingi (base course) km 56 na tabaka la lami km 56, madaraja 32, makalavati makubwa (box culverts) 11 na makalavati madogo (pipe culverts) 172.

43. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa madaraja makubwa unajumuisha kujenga daraja la **Kirumi** kwenye barabara ya Makutano – Sirari, daraja la **Nangoo** kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, daraja la **Sibiti** kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, daraja la **Maligisu** (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi – Maligisu, daraja la **Kilombero** kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge, daraja la **Kavuu** kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga, daraja la **Mbutu** kwenye barabara ya Igunga – Manonga, daraja la **Ruhekei** kwenye barabara ya Mbinga – Mbamba Bay, daraja la **Ruhuhu** kwenye

barabara ya Kitai - Lituhi, daraja la **Momba** katika barabara ya Kibaoni – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo na ununuzi wa *Mabey Compact Emergency Bridge Parts na Crane Lorry*.

Utekelezaji wa ujenzi wa madaraja makubwa hadi kufikia Aprili, 2015 ni kama ifuatavyo:

Daraja la Kirumi

Kazi za mapitio ya usanifu uliofanyika mwaka 2008 zimekamilika. Mapitio ya usanifu yamebaini kuwa nyaya (cables) za daraja zifanyiwe ukarabati badala ya kuweka mpya kama ilivyokuwa imependekezwa hapo awali. Taratibu za kumpata mtaalam wa kuchunguza hali ya nyaya na kupendekeza jinsi ya kuzifanyia ukarabati zinaendelea.

Daraja la Nangoo

Ujenzi wa daraja la Nangoo umekamilika.

Daraja la Sibiti na Barabara zake

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ambazo zimefanyika ni kama ifuatavyo: Ujenzi wa nguzo za msingi wa daraja zimekamilika pamoja na kuanza ujenzi wa makalvati makubwa,

kusafisha eneo la ujenzi wa barabara km 20.2 na ujenzi wa tuta km 19.

Daraja la Maligisu

Ujenzi wa Daraja la Maligisu umekamilika.

Daraja la Mto Kilombero na Barabara zake

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ambazo zimefanyika ni kama ifuatavyo: ujenzi wa tuta km 3.5, ujenzi wa daraja unaendelea, ujenzi wa makalavati madogo (pipe culverts) asilimia 63, ujenzi wa makalavati makubwa (box culverts) unaendelea na ujenzi wa daraja la muda upo asilimia 95.

Daraja la Kavuu

Hadi Aprili, 2015, ujenzi wa msingi na nguzo za daraja hili umefikia asilimia 50.

Daraja la Mbutu

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi za ujenzi wa daraja ulikuwa umekamilika.

Ununuzi wa Mabey Compact Emergency Bridge Parts na Crane Lorry

Ununuzi wa *Mabey Compact Emergency Bridge Parts* upo katika hatua za ununuzi. Ununuzi wa *Crane Lorry* umekamilika.

Daraja la Ruhekei

Ujenzi wa Daraja la Ruhekei umekamilika Septemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

Daraja la Ruhuhu

Kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Ruhuhu yanaendelea.

Daraja la Momba

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

44. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Kawawa JCT – Tegeta)** unahusu ukarabati na upanuzi wa barabara hii yenye urefu wa (km 17.2) kwa kiwango cha lami kutoka njia mbili za sasa kuwa njia nne (4-lane dual carriageway) kutoka Mwenge (Makutano ya Barabara ya Sam Nujoma) hadi Tegeta Kibaoni. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya

Mwenge – Tegeta (km 12.9) na awamu ya pili ni sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3). Kazi za ujenzi na upanuzi wa barabara hii katika awamu ya kwanza zilikamilika Julai, 2014 na mradi huu upo katika kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu kinachotarajiwa kumalizika Julai, 2017.

45. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa barabara ya **Kyaka – Bugene** yenye urefu wa km 59.1 unahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami kutoka Kyaka katika makutano ya barabara ya Mutukula – Bukoba hadi Bugene kupitia makao makuu ya wilaya ya Karagwe ikijumuisha ujenzi wa daraja moja la **Mwisa** pamoja na makalavati. Hadi kufikia Aprili, 2015 hatua za ujenzi zifuatazo zimefikiwa: kujenga tuta la barabara km 54, kujenga tabaka la chini la msingi (sub-base) km 45, kujenga tabaka la msingi (base course) km 43, tabaka la lami km 43, makalavati madogo (pipe culverts) 117, makalavati makubwa (box culverts) 11 na daraja la Mwisa limekamilika.

46. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo (km 392)**, lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242). Aidha, mradi unahusu usanifu wa kina kwa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na Nyakasanza – Kobero (km

59). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa sehemu ya Isaka – Lusahunga. Hadi kufikia Aprili, 2015 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242)

Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili (2) ili kuharakisha utekelezaji: Isaka – Ushirombo (km 132) na Ushirombo – Lusahunga (km 110).

Isaka – Ushirombo (km 132)

Ukarabati wa barabara hii umekamilika Machi, 2014.

Ushirombo – Lusahunga (km 110)

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zilizokamilika ni kama ifuatavyo: ujenzi wa tuta la barabara km 54, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 54, tabaka la lami km 54, makalavati madogo (pipe culverts) 91 na makalavati makubwa (box culverts) 9.

Sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na Nyakasanza – Kobero (59 km)

Kazi za usanifu wa kina zimekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Sekretariati ya

Jumuia ya Afrika Mashariki imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya mapitio ya usanifu zinaendelea.

47. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora** yenye urefu wa kilometa 259.75 ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Chaya – Nyahua (km 85.4) na Nyahua – Tabora (km 85).

Hadi kufikia Aprili, 2015 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)

Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa tuta la barabara km 89.35, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 89.35, tabaka la msingi (base course) km 89.35 na tabaka la lami ni km 88.5.

Tabora – Nyahua (km 85)

Mkandarasi anaendelea na kazi na hatua aliyofikia ni kama ifuatavyo; kujenga tuta la barabara km 70, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 66, tabaka la msingi (base course) km 66 na tabaka la lami km 66.

Chaya – Nyahua (km 85.4)

Mhandisi Mshauri amekamilisha kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa gharama zilizotolewa na Kuwait Fund. Serikali inaendelea na majadliano na Kuwait Fund ili kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

48. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Korogwe – Handeni** yenye urefu wa kilometa 65, lengo ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa barabara hii umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

49. ***Mheshimiwa Spika***, lengo katika barabara ya **Handeni – Mkata** yenye urefu wa kilometa 54 lilikuwa kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi wa barabara hii zilikamilika Novemba, 2012 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kilimalizika Novemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

50. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **barabara za mikoa**, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga kilometa 78 kwa kiwango cha lami, ukarabati wa jumla ya kilometa 685 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja 14. Kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zimefanyika katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu kwa barabara zenye urefu wa kilometa 1,520 ilipangwa kufanyika. Hadi kufikia Aprili, 2015, ujenzi wa km 40.5 kwa kiwango cha lami na ukarabati wa km 450 kwa kiwango cha changarawe umekamilika. Ujenzi wa madaraja uko katika hatua ya ununuzi.

51. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Mwanza/Shinyanga border – Mwanza**, lengo lilikuwa kufanya ukarabati wa sehemu zilizoharibika yenye urefu wa kilometa 10. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi za ukarabati wa sehemu hizo zilizoharibika zinaendelea.

52. **Mheshimiwa Spika**, daraja la Umoja katika mto Ruvuma eneo la Mtambaswala/Negomane limejengwa ili kuunganisha nchi za Tanzania na Msumbiji. Daraja hili lilijengwa kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design and Build). Kazi za ujenzi wa daraja zimekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

53. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam** zenye urefu wa kilometa 109.35. Barabara hizo na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

Ubungo Bus Terminal – Mabibo – Kigogo Roundabout (km 6.4)

Lengo la mradi huu ni kujenga na kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi imekamilika Machi, 2013 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kilimalizika Machi, 2014.

Kigogo Roundabout – Bonde la Msimbazi – Twiga/Msimbazi Jct (km 2.7)

Lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi na kukarabati kwa kiwango cha lami. Mkandarasi ametekeleza kazi kama ifuatavyo: tuta la barabara km 2; tabaka la chini la msingi km 2, tabaka la lami km 2 zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla yamefikia asilimia 75. Kutokamilika kwa wakati kwa kazi za ujenzi zilizobaki kumetokana na zuio la mahakama baada ya wananchi ambao hawakuridhika na viwango vya fidia kufungua kesi mahakamani.

Jet Corner – Vituka – Devis Corner (km 10.30)

Lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi na kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi ulikamilika Septemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Tabata Dampo – Kigogo (km 1.60) na Ubungo Maziwa – External (km 0.65)

Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.60) na Ubungo Maziwa – External (km 0.65). Ujenzi umekamilika kwa sehemu ya Ubungo Maziwa – External. Kwa sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo, ujenzi unaendelea.

Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure – BRT)

Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure – BRT) na vituo vyake upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa Barabara

Mradi unahusisha ujenzi wa barabara ya Morogoro kutoka Kimara hadi Kivukoni, barabara ya Kawawa kutoka Magomeni hadi Morocco na barabara ya Msimbazi kutoka Fire hadi Kariakoo zenye jumla ya urefu wa kilometa 20.9. Pia kuna vituo vya mabasi 29, vituo vikubwa vitatu na madaraja ya waenda kwa miguu matatu.

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zilizofanyika ni kusafisha barabara km 20, tuta la barabara km 20, ujenzi wa madaraja ya waenda kwa miguu unaendelea, ujenzi wa vituo vya mabasi upo asilimia 92, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 20, tabaka la msingi (base course) km 20, tabaka la lami km 20 na barabara ya zege km 20.

Ujenzi wa Karakana (Depot) na Kituo cha Mabasi cha Ubungo

Mradi huu unahusisha ujenzi wa Karakana (Depot), Kituo Kikuu cha Ubungo na uboreshaji wa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo mikoani (Ubungo Up-Country Bus Terminal). Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi bado zilikuwa hazijaanza. Uamuzi umefanyika ili kurejea usanifu baada ya kuondolewa kwa kituo cha

mabasi yaendayo mikoani hivyo taratibu za kutangaza zabuni upya zinaendelea.

Ujenzi wa Karakana (Depot) ya Jangwani

Mradi huu unahusisha ujenzi wa Karakana (Depot) ya Jangwani. Hadi kufikia Aprili, 2015 Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa tabaka la uwekaji wa tuta (Platform), tabaka la chini la msingi (sub-base) asilimia 96, tabaka la zege asilimia 77. Aidha, ujenzi wa jengo la utawala na jengo la ofisi kuu umekamilika.

Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (Terminal) cha Kivukoni

Mradi huu unahusisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kivukoni. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa majengo umefikia asilimia 90. Hata hivyo, mkataba wa awali ulisitishwa Machi, 2014 baada ya Mkandarasi kukiuka baadhi ya vipengele vya mkataba. Kazi zilizobaki zitakamilishwa na mkandarasi mwingine.

Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (Terminal) cha Kariakoo

Mradi huu unahusisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi eneo la Gereza Kariakoo. Kazi haikuanza kama ilivyopangwa kutokana na zuio la mahakama. Baada ya kumaliza tatizo la

kimahakama, Mkandarasi aliyekuwa anafanya kazi hii alikataa kuendelea na mkataba. Aidha, mkataba mpya na Mkandarasi mwingine ulisainiwa tarehe 27 Desemba, 2013 na kazi zilianza tena tarehe 1 Machi, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ya kuchimba msingi wa kituo kikuu cha mabasi imekamilika, kazi ya ujenzi wa msingi wa zege wa kituo cha mabasi na ujenzi wa barabara za maingilio inaendelea.

Ujenzi wa Vituo vya Mlisho (Feeder Stations)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa Vituo Vidogo vya Mabasi, (Urafiki, Shekilango, Magomeni Mapipa, Kinondoni, Mwinyijuma na Fire). Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ya ujenzi wa vituo hivi upo katika hatua za mwisho.

Uhamishaji wa Miundombinu ya Umeme

Mradi huu unahusisha kuhamisha miundombinu ya umeme kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na vituo vya mabasi kwa ajili ya mradi wa usafiri wa Mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam. Kazi za uhamishaji wa miundombinu ya umeme ilikamilika mnamo Agosti, 2011.

Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili – Kinyerezi –Banana (km 14)

Lengo la mradi huu ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu ni sehemu ya

mpango wa Serikali wa kupunguza msongamano wa magari kuingia na kutoka katika barabara za jiji la Dar es Salaam. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ni kutoka Kinyerezi hadi Kifuru (km 4.0). Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi ulikuwa unaendelea.

Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi Mwisho (km 20)

Barabara hii inasaidia magari yanayotokea kaskazini mwa jiji la Dar es Salaam kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na kusini mwa jiji bila kupitia makutano ya Ubungo. Aidha, barabara hii ni kiunganisho cha barabara ya pete (Dar es Salaam Outer Ring Road). Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi ulikuwa unaendelea.

Tangi Bovu – Goba (km 9)

Lengo la mradi huu ni kuijenga barabara ya Tangi Bovu – Goba (km 9) kwa kiwango cha lami ili kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam hususan katika barabara za Bagamoyo na Morogoro. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii ulikuwa unaendelea.

Kimara Baruti–Msewe (km 2.6)

Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kimara – Baruti (km 2.6) kwa kiwango cha lami ili kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam hususan katika barabara ya Morogoro. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii ulikuwa unaendelea.

Kimara – Kilungule – External Mandela Road (km 9)

Lengo la mradi huu ni kuijenga na kufanya upanuzi wa barabara ya Kimara – Kilungule – External (Mandela Road) kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi ulikuwa unaendelea.

Kibamba – Kisopwa (km 12.0)

Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kibamba – Kisopwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii inarahisisha huduma ya usafiri kwenda na kutoka kwenye Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) na Hospitali ya kisasa inayoendelea kujengwa katika eneo la Mlonganzila. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa sehemu ya **Kibamba – Mloganzila** (km 4.0) ulikuwa umekamilika.

54. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa barabara ya **Ndundu – Somanga (km 60)** ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania, Kuwait Fund na OPEC Fund. Mradi huu umekamilika mwezi Novemba, 2014. Mradi upo katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

55. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea** (km 396), lengo la mradi ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kidatu hadi Lumecha/Songea chini ya msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na mchango wa Serikali ya Tanzania. Mkataba wa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umesainiwa Mei, 2014 na kazi zinaendelea.

56. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda** yenye urefu wa kilometa 359 ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mkataba wa sehemu ya **Tabora – Sikonge (Usesula)** yenye urefu wa kilometa 30 umesainiwa na Mkandarasi anaendelea na matayarisho ya kuanza ujenzi. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kutoa mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya

kugharamia ujenzi wa sehemu ya Sikonge (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 329).

57. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (km 239) na Loliondo – Mto wa Mbu (km 213)**, lengo ni kufanya usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Loliondo – Mto wa Mbu (km 213)

Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

Makutano – Natta (km 80): Sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50)

Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** ulikuwa unaendelea.

58. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Ibanda – Itungi/Kiwira (km 26)**, lengo ni kuanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port (km 5.6) kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi wa sehemu ya

Kanjunjumele–Kiwira Port zilianza mwezi Machi, 2015 na kazi zinaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa barabara ya **Tanga – Horohoro** yenye urefu wa kilometa 65, lengo la mradi lilikuwa ni kujenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu uligharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC) ya Marekani na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi wa barabara hii ilikamilika Oktoba, 2012. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha ni kwa ajili ya kulipa fidia.

60. ***Mheshimiwa Spika***, barabara ya **Nzega – Tabora** yenye urefu wa kilometa 115 lengo ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanywa katika sehemu kuu mbili ili kurahisisha utekelezaji kama ifuatavyo: Nzega – Puge (km 58.8) na Puge – Tabora (km 56.10) na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: –

Sehemu ya Nzega – Puge (km 58.8)

Hadi kufikia Aprili, 2015, kazi zifuatazo zilikuwa zimekamilika: kusafisha barabara km 58.8, tuta la barabara km 58.8, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 46, tabaka la msingi (base course) km 44, tabaka la lami km 40 na makalavati makubwa (box culverts) 70.

Sehemu ya Puge – Tabora (km 56.1)

Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Puge – Tabora (km 56.1) ulikuwa umekamilika.

61. ***Mheshimiwa Spika***, barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi** (km 770.9) inaendelea kujengwa kwa awamu. Mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu nne ili kurahisisha utekelezaji: Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36.9) na Mpanda – Uvinza – Kanyani – Nyakanazi (km 582.4). Hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Sumbawanga – Kanazi (km 75)

Kazi zilizofanyika ni kusafisha barabara km 57, tuta la barabara km 47, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 43, tabaka la msingi (base course) km 43 na tabaka la lami km 43, makalavati makubwa (box culverts) na makalavati madogo (pipe culverts) yamekamilika. Mradi unaendelea.

Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6)

Kazi zilizokamilika ni kama ifuatavyo: kusafisha barabara km 76.6, tuta la barabara km 29,

tabaka la chini la msingi (sub-base) km 17, tabaka la juu la msingi (base course) km 16, tabaka la lami km 16, makalavati makubwa (box culverts) 10 na makalavati madogo (pipe culverts) 100. Mradi unaendelea.

Sitalike – Mpanda (km 36.9)

Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa tuta la barabara km 33, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 21, tabaka la juu la msingi (base course) km 21, tabaka la lami km 20, makalavati makubwa (box culverts) 7 na makalavati madogo (pipe culverts) 44. Mradi unaendelea.

Mpanda – Uvinza (km 195.4)

Ujenzi wa barabara hii utafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itahusisha sehemu ya Mpanda–Usimbili kilometa 30. Hadi kufikia Aprili 2015, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami ulikuwa katika hatua za mwisho.

62. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu mradi wa barabara ya **Nyanguge – Musoma (km 183)**, lengo la mradi huu ni kuikarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu pia unahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa

mchepuo wa barabara ya Usagara – Kisesa (km 17), barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda (km 93.5) na barabara ya Nyamuswa – Bunda (km 24.5) kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo: –

Mpakani mwa Simiyu/Mara – Musoma (km 85.5)

Ukarabati ulikamilika Novemba, 2014 na mradi huu upo katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17)

Lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano wa magari katikati ya jiji la Mwanza kwa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unaendelea.

Nansio – Kisorya – Bunda (km 93.5)

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51) unaenendelea.

Nyamuswa – Bunda (km 24.5)

Usanifu wa kina umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyamuswa –

Bunda (km 24.5) utanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

63. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Magole – Mziha (km 83.8)** lengo lake ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili: Magole –Turiani (km 48) na Turiani – Mziha (km 35.8). Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Magole – Turiani (km 48.8)

Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zilizokamilika ni kama zifuatazo: ujenzi wa tuta la barabara km 40.7, tabaka la chini la msingi (sub - base) km 13.8, tabaka la msingi (base course) km 13.8, tabaka la lami km 13.8, ujenzi wa madaraja matatu (3) na ujenzi wa makalavati makubwa na madogo umekamilika.

Mziha – Turiani (km 35.8)

Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami katika sehemu hii ya barabara.

64. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ujenzi **wa barabara za juu (flyovers) na**

maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam, lengo la mradi ni kujenga ‘Flyover’ ya TAZARA, “Interchange” ya Ubungo na maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Hadi Aprili, 2015 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Barabara ya Juu (*Flyover*) ya TAZARA

Usanifu wa kina ulikamilika katika mwaka wa fedha 2013/14 chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi hazikukamilika mapema kutokana na bei za zabuni kuwa juu ya bajeti iliyopangwa awali. Taratibu za ununuzi zinaendelea huko Japan kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayekidhi vigezo. Kazi ya ujenzi wa *Flyover* ya TAZARA ambayo itagharamiwa na Serikali ya Japan inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2015.

***Interchange* ya Ubungo**

Benki ya Dunia imekubali kugharamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) katika makutano ya Ubungo. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina *Interchange* ya Ubungo umekamilika. Zabuni ya

kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi zimetangazwa. Aidha, Serikali inakamilisha taratibu kwa ajili ya kutangaza zabuni za kumtafuta Mkandarasi wa ujenzi. *Interchange* ya Ubungo itakuwa na *levels* tatu ambapo magari yanayotoka katikati ya jiji la Dar es Salaam kuelekea Morogoro yatapita chini, magari yanayotoka TAZARA kuelekea Mwenge yatapita juu na magari yanayokata kulia yatapita katikati.

Maboresho ya Makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu na Morocco

Maandalizi kwa ajili ya maboresho ya makutano yaliyoainishwa yanaendelea.

65. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Bariadi – Lamadi (km 71.8)**, lengo la mradi huu ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi (km 171) na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zilizofanyika kwa sehemu ya **Bariadi – Lamadi (km 71.8)** ni kusafisha barabara (clearing and grubbing) km 68, ujenzi wa tuta km 65, tabaka la msingi (sub - base) km 65, tabaka la msingi (base course) km 65, tabaka la chini la lami km 65 na madaraja makubwa matatu (3) yamefikia

asilimia 95, makalavati makubwa (box culverts) 19 na makalavati madogo (pipe culverts) 68. Aidha, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Mwigumbi – Maswa (km 50)** umesainiwa na mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

66. **Mheshimiwa Spika**, barabara ya **Ipole – Rungwa (km 112)**, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mkataba wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa Desemba, 2014 na kazi zinaendelea.

67. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310)**, lengo ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusu sehemu ya Nyakanazi – Kibondo yenye urefu wa kilometa 50 na sehemu ya Kidahwe – Kasulu yenye urefu wa kilometa 50. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mikataba ya ujenzi kwa sehemu zote mbili imesainiwa na Makandarasi wameanza kazi za ujenzi wa barabara hii.

68. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa barabara ya kwenda **Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Airport Access Road)** yenye urefu wa kilometa 14, lengo lilikuwa kuijenga kwa

kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na umekamilika mwezi Januari, 2015.

69. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (Dodoma University Road)** yenye urefu wa km 12 una lengo la kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2015 mradi ulikuwa unaendelea.

70. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa ujenzi wa **daraja la Kigamboni** unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Lengo la mradi huu ni kujenga daraja lenye urefu wa mita 680 na barabara unganishi za kilometa 2.5. Daraja hili litaunganisha Jiji la Dar es Salaam na eneo la Kigamboni. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa daraja umekamilika kwa asilimia 80.

71. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la barabara ya **Sam Nujoma** lilikuwa ni kupanua kutoka njia mbili kuwa njia nne pamoja na njia za waenda kwa miguu kuanzia Mwenge hadi Ubungo. Mradi huu umegharamiwa na Serikali ya Tanzania na kazi ya ujenzi wa barabara ilikamilika Julai, 2009. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya Mkandarasi.

72. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ukanda wa Kati** (Central Corridor) una lengo la kuimarisha na kuboresha barabara pamoja na kuongeza usalama kwa watumia barabara katika ukanda huo. Hadi kufikia Aprili, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa maeneo yanayohitaji kuimarishwa na kuboreshwa zilikuwa zinaendelea.

73. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa barabara ya **Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) hadi Pugu (km 8.0)** ni kuipanua barabara hii kuwa njia sita. Hadi kufikia Aprili, 2015 taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina zinaendelea.

74. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusu kuipanua kuwa njia sita. Aidha, mradi unajumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Maandalizi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina yanaendelea.

75. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa barabara ya **Kisarawe – Mlandizi (km 52)** ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Maandalizi ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina yanaendelea.

76. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi wa **barabara za Bandari (km 1.2), barabara ya Dockyard (km 0.7) na Mivinjeni (km 1.0)** ni kupanua sehemu ya barabara hizi ili kukidhi mahitaji ya magari makubwa yanayoingia na kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam. Hadi kufikia Aprili, 2015 maandalizi ya kufanya usanifu wa kina yanaendelea.

77. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, lengo la mradi ni kupanua kuwa njia sita. Mradi huu unatekelezwa katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na sehemu ya pili ni Mbezi Mwisho – Kifuru – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3) ambao unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2015 taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hii ulikuwa unaendelea.

78. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa **mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam**, lengo ni kujenga mizani ya kisasa ili madereva wa magari makubwa wapime uzito wa mzigo waliobeba kabla ya kuanza safari

na hivyo kukidhi tatizo la uzidishaji wa mizigo kwenye malori makubwa. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

79. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Tunduma – Sumbawanga (km 222.8)** ni kuboresha miundombinu ya barabara katika Ukanda wa Magharibi. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Changamoto za Milenia (MCC) na mchango wa Serikali ya Tanzania. Mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu (3) na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

Tunduma – Ikana (km 63.7)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Novemba, 2013.

Ikana – Laela (km 64.2)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Oktoba, 2013.

Laela – Sumbawanga (km 93.3) na Tunduma Township (km 1.6)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Februari, 2015.

80. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga (km 154)** ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Biharamulo – Lusahunga (km 294). Ujenzi wa sehemu ya barabara ya Mutukula – Muhutwe – Kagoma ulikamilika Septemba, 2004 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa OPEC. Kwa upande wa sehemu ya Kagoma – Lusahunga (km 154), ujenzi ulikamilika Desemba, 2013 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kilimalizika Novemba, 2014. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

81. **Mheshimiwa Spika**, barabara ya **Arusha – Namanga (km 105)** ni sehemu ya mradi wa kikanda wa Arusha – Namanga – Athi River (km 241) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaojumuisha nchi za Tanzania na Kenya ambao ulifadhiliwa na *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kushirikiana na Serikali za Tanzania na Kenya. Lengo la mradi huu ni kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu ulikamilika Desemba, 2012 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kimekamilika. Aidha, mradi huu ulijumuisha ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (One Stop Border Post) cha Namanga ambacho pia kimekamilika. Fedha zilizotengwa

katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

82. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **barabara ya Arusha – Minjingu – Babati – Singida** yenye urefu wa kilometa 327.5, lengo la mradi ni kuijenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Minjingu – Babati – Singida (km 223.5) kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kwa sehemu ya Minjingu – Arusha (km 104) lengo lilikuwa kuifanyia ukarabati sehemu hii ya barabara kwa kiwango cha lami kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Singida – Kateshi (km 65.1)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Februari, 2012.

Kateshi – Dareda (km 73.8)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Agosti, 2012.

Dareda – Babati – Minjingu (km 84.6)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Agosti, 2012.

Minjingu – Arusha (km 104)

Ukarabati ulikamilika Septemba, 2014.

Fedha zilizotengwa kwenye mradi huu ni za kulipa sehemu ya madai ya makandarasi.

83. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road)** yenye urefu wa kilometa 12.9, lengo ni kukarabati na kupanua barabara ya lami kutoka njia mbili hadi nne kati ya Bendera Tatu na Mbagala Rangi Tatu na Bendera Tatu – KAMATA kwa msaada kutoka Serikali ya Japan. Utekelezaji wa mradi huu ni kuwa, kazi ya ujenzi sehemu ya Mbagala Zakhem mpaka Mbagala Rangi Tatu (km 1.5) ulikamilika Aprili, 2012. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu – KAMATA (km 1.3) unaendelea kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipia fidia na kuondoa miundombinu ya maji na umeme.

84. **Mheshimiwa Spika**, barabara ya **Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga – Igawa (km 367.4)** lengo lilikuwa ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Iyovi – Kitonga Gorge (km 86.3),

Ikokoto – Iringa (km 60.9), barabara ya mchepuo kuingia Iringa mjini (km 2.1), Iringa–Mafinga (km 69.4) na Mafinga – Igawa (km 137.9) katika barabara kuu ya Dar es Salaam – Tunduma (TANZAM). Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto – Iringa/Mchepuo wa Kuingia Iringa Mjini (km 149.3)

Ukarabati ulikamilika Septemba, 2011. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni za kulipa madai ya Mkandarasi.

Iringa – Mafinga (km 69.4)

Ukarabati ulikamilika Agosti, 2013. Kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kimeisha Agosti, 2014. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni za kulipa madai ya Mkandarasi.

Mafinga – Igawa (km 146.0)

Ukarabati wa barabara hii umegawanywa katika sehemu mbili: Mafinga – Nyigo (km 74.1) na Nyigo – Igawa (km 63.8). Mikataba ya ujenzi kwa ajili ya Mafinga – Nyigo km 74.1 na Nyigo – Igawa (km 63.8) imesainiwa na maandalizi ya kuanza ukarabati yanaendelea. Mradi huu

utagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

85. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi wa ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) ni kujenga barabara hii kwa lami***. Usanifu wa kina umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

86. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya ***Njombe – Ndulamo – Makete (km 109)*** ni kuboresha mawasiliano ya barabara kati ya Makao Makuu ya Mkoa wa Njombe na Makao Makuu ya Wilaya ya Makete. Ujenzi kwa kiwango cha lami umeanza na utaendelea katika mwaka wa fedha 2015/16.

87. ***Mheshimiwa Spika***, mradi barabara ya ***Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)*** umegawanyika katika sehemu mbili: Korogwe – Mkumbara (Km 76) na Mkumbara – Same (Km 96) na unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Utekelezaji wa miradi hii hadi kufikia Aprili, 2015 ni kama ifuatavyo:

Korogwe – Mkumbara (km 76)

Ukarabati umekamilika Desemba, 2014 na mradi huu uko katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

Mkumbara – Same (km 96)

Kazi zilizokamilika ni kama zifuatazo: ujenzi wa tuta la barabara km 68, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 61, tabaka la msingi (base course) km 59 na tabaka la lami km 58, makalavati makubwa (box culverts) 22 na makalavati madogo (pipe culverts) 100.

88. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya ***Mbeya – Makongolosi (km 115)***, lengo ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 43). Kwa sehemu ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 413), lengo ni kufanya usanifu wa kina. Hadi kufikia Aprili, 2015 hatua za utekelezaji zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:

Mbeya – Lwanjilo (km 36)

Kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 36, tabaka la chini la msingi (sub-base) km 24, tabaka la msingi (base course) km 23, tabaka la lami km 23, makalavati makubwa (box culverts) 2 na makalavati madogo (pipe culverts) 90.

Lwanjilo – Chunya (km 36)

Ujenzi umekamilika Desemba, 2014 na mradi huu upo katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

Chunya – Makongolosi (km 43)

Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 413)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inatafuta fedha za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

89. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la barabara ya ***Chalinze – Segera – Tanga (km 245)*** ni kuifanyia ukarabati na upanuzi. Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu uligawanywa katika sehemu mbili ambazo ni: Chalinze – Kitumbi (km 125) na Kitumbi – Segera – Tanga (km 120).

Hadi Aprili, 2015 utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Chalinze – Kitumbi (km 125)

Ujenzi wa sehemu hii ulikamilika Oktoba, 2010. Kipindi cha uangalizi kilitakiwa kumalizika mwezi Oktoba, 2011. Kipindi hicho kiliongezwa kwa miaka miwili zaidi baada ya kuonekana barabara ina kasoro za ubora zilizojitokeza. Hata hivyo, barabara hii bado haijapokelewa kwa sababu kasoro za ubora zilizojitokeza zinaendelea kurekebisha na Mkandarasi kwa gharama zake.

Kitumbi – Segera – Tanga (Km 120)

Ukarabati umekamilika Machi, 2014.

Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass) (km 10)

Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika Januari, 2015.

90. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu **daraja jipya la Ruvu Chini (Lower Ruvu Bridge)**, lengo la mradi huu ni kujenga daraja jipya katika Mto Ruvu kwenye barabara ya Bagamoyo – Msata. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa daraja la Ruvu chini unaendelea chini ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata.

91. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda (km 211)** unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi Aprili, 2015 taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

92. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Dodoma – Mtera – Iringa (km 260)**, lengo ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA). Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni Iringa – Migori (km 95.2); Migori – Fufu Escapment (km 93.8) na Fufu Escapment – Dodoma (km 70.9). Hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji wa mradi huu ni kama ifutavyo:

Iringa – Migori (km 95.2)

Kazi zilizokamilika ni kama zifuatazo:– kusafisha eneo la ujenzi km 95.2, kujenga tuta la barabara km 95.2, kujenga tabaka la chini la msingi (sub-base) km 95.2, kujenga tabaka la juu (base course) km 95.2, kujenga tabaka la lami km 77.3, ujenzi wa makalavati makubwa (box culverts) 56 na makalavati madogo (pipe culverts) 206.

Migori – Fufu Escarpment (km 93.8)

Ujenzi umekamilika Januari, 2015 na mradi uko katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.9)

Ujenzi umekamilika Julai, 2014 na mradi huu uko katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.

93. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa barabara ya **Dodoma – Babati** yenye urefu wa kilometa 261, lengo ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Serikali ya Tanzania. Mradi umegawanywa katika sehemu nne: Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela - Bonga (km88.8) na Bonga – Babati (km 19.2). Hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Dodoma – Mayamaya (km 43.65)

Kazi zilizokamilika ni: kujenga tuta la barabara km 37, kujenga tabaka la chini la msingi (sub - base) km 35, kujenga tabaka la msingi (base course) km 35, tabaka la lami km 35 mradi unaendelea.

Mayamaya – Mela (km 99.35)

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa Desemba, 2013. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA). Hadi Aprili, 2015 kazi zifuatazo zimefanyika: kusafisha eneo la ujenzi km 80, ujenzi wa tuta km 20, makalavati makubwa (box culverts) 11 na makalavati madogo (pipe culverts) 54. Ujenzi unaendelea.

Mela – Bonga (km 88.80)

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa Desemba, 2013. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA). Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zifuatazo zimekamilika: kusafisha eneo la barabara km 34 na kujenga tuta km 15. Ujenzi unaendelea.

Bonga – Babati (km 19.2)

Ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Aprili, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

94. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Mtwara – Mingoyo – Songea – Mbamba Bay (km 819) na Songea – Makambako (km 295)** lengo lake ni kuboresha miundombinu ya barabara kwenye Ukanda wa Mtwara (Mtwara Corridor). Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika sehemu za Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200), Masasi – Mangaka (km 54), Mangaka – Mtambaswala (km 65.5), Mangaka – Nakapanya – Tunduru (km 146), Tunduru – Matemanga (km 58.7), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60.7); Namtumbo – Songea (km 72), Peramiho Jct – Mbinga (km 78), Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Masasi – Newala – Mtwara (km 209) na Songea – Makambako (km 295).

Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya barabara hii.

Masasi – Mangaka (km 54)

Awamu ya kwanza km 15 ya mradi ilikamilika Machi, 2009. Awamu ya pili km 17.6 ya mradi ilikamilika Machi, 2010. Awamu ya Tatu km

22.5 nayo ilikamilika Desemba, 2011. Barabara hii imejengwa kwa msaada wa Serikali ya Japan.

Mangaka – Mtambaswala (km 65.50)

Mkataba ujenzi wa sehemu hii ulisainiwa Desemba, 2013. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Misaada la Japan (JICA). Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa unaendelea.

Mangaka – Nakapanya (km 70.50)

Mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Mangaka – Nakapanya ulisainiwa Februari, 2014. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA). Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa unaendelea.

Nakapanya – Tunduru (km 66.50)

Mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Nakapanya – Tunduru ulisainiwa Februari, 2014. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA).

Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa unaendelea.

Tunduru – Matemanga (km 58.7)

Mkataba wa awali ulisitishwa Januari 2013 kutokana na utendaji usiyoridhisha wa Mkandarasi. Hivyo, mkataba mpya wa ujenzi ulisainiwa Februari, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa unaendelea kwa fedha za mkopo kutoka AfDB na JICA.

Matemanga – Kilimasera (km 68.2)

Mkataba wa awali ulisitishwa Januari 2013 kutokana na utendaji usiyoridhisha wa Mkandarasi. Mkataba mpya wa ujenzi ulisainiwa Aprili, 2014 na kazi za ujenzi zinaendelea kwa fedha za mkopo kutoka AfDB na JICA. Hadi Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa unaendelea.

Kilimasera – Namtumbo (km 60.7)

Mkataba wa awali ulisitishwa Januari 2013 kutokana na utendaji usiyoridhisha wa Mkandarasi. Mkataba mpya wa ujenzi ulisainiwa Februari, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikuwa

unaendelea kwa fedha za mkopo kutoka AfDB na JICA.

Namtumbo – Songea (km 72)

Ujenzi ulikamilika Novemba, 2013.

Peramiho Jct – Mbinga (km 78)

Ujenzi ulikamilika Novemba, 2013.

Mbinga – Mbamba Bay (km 66)

Usanifu wa kina wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) umekamilika. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kuipatia Serikali ya Tanzania mkopo kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) inakamilisha taratibu za kutangaza zabuni ya ujenzi.

Mtwara – Newala – Masasi (km 209)

Mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa Mei, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa kina wa barabara hii ulikuwa umekamilika. Taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Mtwara – Nanyamba (km 60) zipo katika hatua za mwisho.

Songea – Makambako (km 295)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii.

95. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) una mpango wa kujenga **Makao Makuu ya Wakala wa Barabara** pamoja na Ofisi za mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za ndani. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa jengo la Makao Makuu ya Wakala ulikuwa umekamilika. Maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala na Ofisi za mikoa yanaendelea.

96. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu barabara ya **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo**, lengo ni kujenga barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye Chuo cha Uongozi kilichopangwa kujengwa Bagamoyo pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho. Usanifu wa kina wa barabara hii ulikamilika Oktoba, 2014. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

97. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS imeendelea **kuzifanyia**

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ikiwa ni maandalizi ya kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara hizo. Hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

Barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Saadani –Pangani – Tanga (km 178)

Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Tanga kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kama sehemu ya mradi wa kikanda wa Malindi – Mombasa – Lunga Lunga/Tanga – Bagamoyo kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hii.

Barabara ya Sumbawanga – Kasesya/Matai – Kasanga Port (km 162): Sehemu ya Matai – Kasesya (km 50)

Lengo la mradi huu ni kufanya usanifu wa kina wa sehemu ya Matai-Kasesya (km 50) ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya usanifu wa kina wa barabara hii imeanza Julai, 2014 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

Barabara ya Ifakara – Mahenge (km 67)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kama sehemu ya mradi wa barabara ya Kidatu–Ifakara–Lupilo–Malinyi–Lumecha (Songea) chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa Nyaraka za Zabuni zilianza Juni 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa kina ulikuwa unaendelea.

Barabara ya Kibondo – Mabamba (km 35)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kazi hiyo umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza Mei, 2014 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

Baarabara ya Mpemba – Isongole (km 49)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika Machi, 2015. Ujenzi kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kazi hii umesainiwa Julai, 2014 na usanifu wa kina unatarajiwa kukamilika Agosti, 2015.

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco (km 178): Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco (km 124)

Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco yenye urefu wa kilometa 178. Barabara hii imepangwa kujengwa kwa awamu. Awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1). Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami inaendelea. Awamu ya pili itahusu upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ujenzi wa sehemu ya barabara kutoka Bugene hadi Kasulo/Benaco yenye urefu wa kilometa 124. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mkataba umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu zinaendelea.

Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Goima – Chemba – Kwamtoro – Singida (km 460)

Lengo la mradi huu ni kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Handeni – Kiberashi – Kondoa kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni inaendelea.

Barabara ya Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 16.9)

Lengo la mradi huu ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mbezi (Morogoro road) – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 16.9). Ujenzi wa barabara hii unalenga kupunguza msongamano wa magari yanayoingia na kutoka katika Jiji la Dar es Salaam. Kazi za ujenzi kwa awamu ya kwanza kutoka Kinyerezi hadi Kifuru (km 4.0) zinaendelea. Kazi za ujenzi katika awamu ya pili kwa sehemu ya Kifuru – Mbezi (Morogoro Road, km 12.9) zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/16.

Daraja Jipya Katika Mto Wami

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na utayarishaji wa

nyaraka za zabuni kwa ajili ya kujenga daraja jipya katika mto Wami kwenye barabara ya Chalinze – Sogera ili kuboresha usalama katika daraja hilo. Mkataba umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja ilianza Mei, 2014 na imekamilika. Serikali inatafuta fedha za kuanza kujenga daraja hili.

Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza Juni, 2014. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa kina ulikuwa unaendelea.

Fidia (Compensation) ya TAZARA Flyovers

Lengo la mradi huu ni kulipa fidia kwa mali na kuhamisha miundombinu ya huduma za kijamii zitakazoathirika na ujenzi wa “flyover” katika eneo la TAZARA. Utaratibu wa kuhamisha miundombinu ya huduma za kijamii zitakazoathirika na ujenzi wa “flyover”

unaendelea. Ujenzi wa “flyover” katika eneo la TAZARA unatarajiwa kuanza Juni, 2015.

Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 209)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza Juni, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa kina wa barabara hii ulikuwa umekamilika.

Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuji – Matala – Oldeani Jct (km 328)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba umesainiwa na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza Julai, 2014 na zinatarajiwa kukamilika Machi, 2016.

Barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 149)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015

kazi ya upembuzi yakinifu ilikuwa imekamilika na kazi ya usanifu wa kina ilikuwa inaendelea.

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa Februari, 2014. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi ya usanifu wa kina ilikuwa imekamilika.

Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Hadi kufikia Aprili, 2015, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

Musoma – Makojo – Busekela (km 92)

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Hadi kufikia Aprili, 2015 usanifu wa kina ulikuwa unaendelea.

Vifaa vya Maabara, Ufuatiliaji na Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara (Central Materials Laboratory – CML)

Lengo la mradi huu ni ununuzi wa vifaa vya maabara, usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa miradi ya barabara ili kuhakikisha ujenzi huo unakidhi viwango vilivyowekwa. Taratibu za ununuzi wa vifaa vya maabara zinaendelea.

Kupanua Barabara Kwenye Miinuko Mikali Katika Barabara Kuu

Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa upanuzi wa sehemu zenye miinuko mikali katika barabara kuu. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

Kuboresha Mwongozo wa Usanifu wa Barabara (Road Geometric Design Manual) na Mwongozo wa Tathmini za Kiuchumi (Economic Appraisal Manual)

Kazi ya kuandaa Mwongozo wa Usanifu wa Barabara (Road Geometric Design Manual) imekamilika na mwongozo umeanza kutumika. Aidha, kazi ya kuandaa Mwongozo wa Tathmini za Kiuchumi (Economic Appraisal Manual) kwa miradi ya barabara nayo imekamilika mwezi Machi, 2015.

Ujenzi na Ukarabati wa Miradi ya Barabara za Mikoa

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya ukarabati wa jumla ya kilometa 914.80 kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometa 94 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2015 jumla ya kilometa 450 zilikuwa zimefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kilometa 40.5 kwa kiwango cha lami.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho ya Vivuko na Matengenezo ya Magari

98. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ilipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Ununuzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kigamboni na Magogoni na kivuko kingine kitakachotoa huduma kati ya Pangani na Bweni mkoani Tanga.
- (ii) Ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Mwanza, MV Kiu (Kilombero), MV Pangani II pamoja na kumalizia ukarabati wa kivuko cha MV Magogoni.
- (iii) Ununuzi wa mashine za kielektroniki za ukatishaji tiketi katika vituo vya Kisorya– Rugezi (Mara/Mwanza), Pangani – Bweni (Tanga) na Ilagala – Kajeje (Kigoma).
- (iv) Ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli (Geita), Iramba – Majita (Mara) na Dar es Salaam – Bagamoyo (Magogoni na Jangwani Beach).
- (v) Matengenezo ya magari ya Serikali katika karakana zote za kila Mkoa.
- (vi) Ujenzi wa vituo vya abiria kwa kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo katika

maeneo ya Magogoni na Jangwani Beach na maandalizi ya kuanzisha usafiri wa majini katika mwambao wa Ziwa Victoria ili kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Mwanza.

- (vii) Ukarabati wa karakana za MT Depot (Dar es Salaam) na Dodoma pamoja na ununuzi wa vifaa vya karakana sita (6) ambazo ni Manyara Singida, Lindi, Mwanza, Kagera na Ruvuma.
- (viii) Kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

99. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Wizara ya Ujenzi kupitia TEMESA imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni na kivuko cha Pangani – Bweni zipo katika hatua za mwisho.
- (ii) Taratibu za kumpata mkandarasi wa kukarabati kivuko cha MV Magogoni zipo katika hatua za mwisho
- (iii) Taratibu za ununuzi wa mashine za kielektroniki za kukatia tiketi katika Kivuko cha Ilagala – Kajeje zinaendelea.

- (iv) Ujenzi wa maegesho ya Iramba – Majita unaendelea. Aidha, ujenzi wa maegesho ya kivuko kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo eneo la Magogoni na Mbegani umekamilika na kivuko kinafanya kazi.
- (v) Jumla ya magari 10,991 yalifanyiwa matengenezo katika karakana za mikoa yote.
- (vi) Ujenzi wa vituo vitatu vya maegesho ya kivuko cha MV TEMESA katika maeneo ya Luchelele, Igogo na Sweya kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari jijini Mwanza unaendelea.
- (vii) Ukarabati wa karakana za MT. Depot na Dodoma unaendelea. Ujenzi wa karakana mpya ya mkoa wa Manyara unaendelea.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

100. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo (TBA) ilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea pamoja na kununua viwanja zaidi mikoani ili kuuwezesha Wakala kujenga nyumba nyingi zaidi za Watumishi wa umma Mikoani; kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalam kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za Watumishi na ofisi za Serikali na

kwa kuzingatia mahitaji na matakwa ya watu wenye ulemavu; kuendelea na mradi maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 za Watumishi wa umma; kuendelea kuimarisha Kikosi cha Ujenzi cha Wakala kwa kutoa mafunzo na kununua vifaa na kuanza ujenzi wa nyumba 149 za TAMISEMI.

101. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015, TBA imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya viongozi na watumishi wa umma, majengo ya ofisi za Serikali na majengo ya biashara ambapo utekelezaji wa miradi ifuatayo upo katika hatua za umaliziaji: ujenzi wa jengo la ghorofa 8 lenye ‘flats’ 16 lililopo eneo la SIDA Estate (Dar es Salaam); jengo la ghorofa 4 lililopo eneo la Mbezi Beach EX – NMC (Dar es Salaam); jengo la kitega uchumi lililopo barabara ya Wachaga (Arusha) na jengo la ghorofa 6 lililopo mtaa wa Moshi (Dodoma). Aidha, Wakala umesimamia jumla ya miradi 58 ya Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Umma ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Usanifu wa miradi hii umezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Vile vile, Wakala umeendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi ambapo umekamilisha ujenzi wa nyumba 155 zilizopo eneo la Bunju B, Dar es Salaam. Wakala pia umeendelea kuimarisha Kikosi chake cha ujenzi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya “Tunnel

Formwork System” ili kuongeza kasi ya ujenzi na kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za watumishi wa Serikali. Kwa upande wa ujenzi wa nyumba za TAMISEMI, Wakala umeanza ujenzi wa nyumba 149 katika mikoa 20 ya Tanzania Bara ambapo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali.

Usalama Barabarani na Mazingira

102. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi iliendelea kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa mizani ya kisasa katika maeneo ya Vigwaza na Mikese ambayo itapima uzito wa magari yakiwa katika mwendo (Weigh in Motion); ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Stations – OSIS) katika Ukanda wa Kati; uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani (National Road Safety Agency) na kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine iliyopangwa ni mradi wa kuweka mfumo wa upatikanaji na utoaji wa taarifa zinazohusu ajali za barabarani. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ilipanga kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 kwa miradi inayotekelezwa katika Sekta ya Ujenzi.

103. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 utekelezaji wa kazi za Usalama Barabarani na Mazingira ulikuwa unaendelea vizuri. Wizara imekamilisha ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa katika mwendo (Weigh-In-Motion) katika eneo la Vigwaza mkoani Pwani. Kufuatia kukamilika kwa mizani hiyo, kituo cha mizani cha Kibaha kimefungwa na hivyo kupunguza kero ya msongamano wa magari katika eneo hilo. Aidha, kazi ya ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa katika mwendo katika eneo la Mikese mkoani Morogoro inaendelea.

Kuhusu ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja vya Muhalala (Manyoni) na Nyakanazi, mradi upo katika hatua ya usanifu wa kina. Ujenzi wa mradi huu umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2015/16. Kwa upande wa uanzishwaji wa Wakala wa Usalama Barabarani (National Road Safety Agency), Serikali imeamua kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani (National Road Safety Authority) ili iwe na mamlaka zaidi ya kisheria kusimamia majukumu ya usalama barabarani. Hadi kufikia Aprili, 2015 taratibu za kuanzisha Mamlaka hiyo zilikuwa zinaendelea. Aidha, mradi wa kuweka mfumo wa upatikanaji na utoaji wa taarifa zinazohusu ajali za barabarani upo katika hatua za mwisho.

Kuhusu masuala ya usimamizi wa mazingira, hadi kufikia Aprili, 2015 Wizara ilikuwa inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika Sekta ya Ujenzi.

UTEKELEZAJI WA MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara

104. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilipanga kutekeleza kazi mbalimbali zenye lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara, zikiwa ni pamoja na; kuendelea na kazi ya maandalizi ya Mwongozo wa Ushiriki wa Wanawake katika Kazi za Barabara, kutembelea shule 5 za sekondari za wasichana ili kuwashawishi waweze kusoma masomo ya sayansi yatakayowasaidia kusomea fani za uhandisi pamoja na kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake kuhusu namna ya kuandaa zabuni na kufanya makisio ya gharama za kazi. Hadi kufikia Aprili, 2015 kazi zilizofanyika ni kuitisha mkutano wa wadau kwa ajili ya kupitia na kuboresha rasimu ya Mwongozo wa Ushirikishaji wa Wanawake katika kazi za barabara. Ukamilishaji wa Mwongozo huo upo katika hatua za mwisho.

Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa

105. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda na hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

106. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara imeshiriki katika kuandaa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu iliyoidhinishwa mwaka 2012 na Wakuu wa Nchi za EAC ambayo inajumuisha miradi ya barabara inayounganisha Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Taarifa hiyo ilipokelewa na kujadiliwa na kikao cha Wakuu wa Nchi za EAC kilichofanyika Nairobi Novemba, 2014.

107. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kushiriki katika maandalizi ya kutunga Kanuni za Udhibiti wa Uzito wa Magari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari katika Jumuiya (EAC Vehicle Load Control Act, 2013).

108. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

(SADC), Wizara ilishiriki katika mikutano mbalimbali ukiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Agosti, 2014 nchini Zimbabwe ambapo Mkakati Elekezi wa Maendeleo (*Regional Indicative Strategic Development Plan – RISDP*) kwa kipindi cha 2015–2020 ulijadiliwa. Mkakati huo unaainisha masuala ya vipaumbele na eneo mojawapo ni uendelezaji wa miundombinu ya kuchochea mtangamano katika kuleta maendeleo ya biashara na uchumi kwa nchi wanachama.

109. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia iliendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Kuendeleza Miundombinu (*Regional Infrastructure Development Master Plan – RIDMP*). Lengo la Mpango huu ni kuwa na miundombinu ya uhakika itakayoziunganisha nchi wanachama na hatimaye kupunguza gharama za usafirishaji na kurahisisha ufanyaji wa biashara kwa nchi wanachama. Miradi ya barabara inayojumuishwa katika Mpango Kamambe ni kama ifuatavyo: Dar es Salaam – Chalinze *Expressway* (km 100), barabara ya Mtwara – Mbamba Bay sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66), TANZAM Highway sehemu ya Makambako – Songea (km 295) na barabara ya Manyoni – Tabora – Kigoma sehemu za Nyahua – Chaya (km 90) na Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (km 310).

Maendeleo ya Watumishi

110. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka watumishi 8 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 46 katika mafunzo ya muda mfupi. Kati ya watumishi hao, 43 walipewa mafunzo ndani ya nchi na 3 walipata mafunzo nje ya nchi. Watumishi 34 waliajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni, watumishi 25 walipandishwa vyeo, 5 walibadilishwa vyeo na 9 walithibitishwa kazini.

Mapitio ya Sera ya Ujenzi

111. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Ujenzi ilipanga kufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 ili iweze kukidhi mazingira ya sasa. Hadi kufikia Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekamilisha rasimu ya Sera na Mkakati wake wa utekelezaji.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

112. **Mheshimiwa Spika**, utoaji wa huduma kwa kutumia TEHAMA ni moja kati ya vipaumbele vya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliendelea kutoa huduma

na taarifa mbalimbali kwa wananchi kwa kupitia tovuti ya Wizara. Mradi wa utengenezaji wa mfumo wa kuweka taarifa za ajali za barabarani unaotumia TEHAMA (Road Accident Information System) ulikamilika. Aidha, Wizara ilikamilisha mfumo wa utoaji wa vibali vya mizigo isiyo ya kawaida barabarani kwa njia ya kielektroniki (Abnormal Load Permit System) ili kurahisisha huduma hiyo kwa wasafirishaji. Wizara pia imeendelea kushiriki katika mafunzo na mikutano mbalimbali inayolenga kuboresha matumizi bora na sahihi ya TEHAMA Serikalini.

Mawasiliano kwa Umma

113. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu masuala yanayohusu sekta ya ujenzi. Wizara pia iliandaa machapisho likiwemo Jarida litwalo *Ujenzi Newsletter* pamoja na kushiriki kwenye maonesho mbalimbali kwa madhumuni ya kutoa elimu kwa umma. Aidha, Wizara iliandaa na kurusha vipindi maalum vya matukio mbalimbali kwenye televisheni, radio, tovuti ya Wizara na mitandao ya kijamii. Vipindi hivyo vilihusu kazi za ujenzi wa barabara, vivuko, nyumba za Serikali pamoja na masuala ya usalama barabarani.

UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

114. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 751.7 na kuzigawanya kwenda Wizara ya Ujenzi, TANROADS na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Aidha, Bodi ilipanga kuandaa na kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuongeza mapato ya Mfuko kwa kupendekeza vyanzo vipya vya mapato na marekebisho ya tozo kwa vyanzo vilivyopo; kuendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, TANROADS, EWURA na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufuatilia na kuweka mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato kwenye vyanzo vya mapato ya Mfuko; kuandaa mapendekezo ya kuboresha vipengele katika sheria iliyoanzisha Bodi ili kuboresha ufanisi wa utendaji wa Taasisi za barabara (Road Authorities) na kutoa adhabu kali kwa watendaji wanaohusika na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko; kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Mfuko wa Barabara (Regulations) na miongozo mbalimbali ili kuboresha usimamizi wa Fedha za Mfuko. Vile vile, Bodi ilipanga kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za

Mfuko kwa kutumia wataalam washauri na wataalam wa ndani kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kiufundi wa ubora wa kazi (value for money) katika mikoa yote nchini wakati miradi ya matengenezo ya barabara inaendelea; kushirikiana na TANROADS kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kupima uzito wa magari kwenye vituo vya mizani na kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ya mizani na kuimarisha mfumo wa mawasiliano (Management Information System); kuendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo wa sekta ya barabara kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za barabara; kuweka Mfumo wa mawasiliano (Management Information System) ili kuboresha utendaji kazi za Bodi na kupitia Mpango Mkakati wa Bodi ya Mfuko ili uendane na mahitaji ya hivi sasa.

115. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Bodi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ilipanga kufanya utafiti wa maeneo mapya yanayoweza kutumika kama tozo kwa ajili ya mfuko kwa lengo la kupanua wigo wa mfuko. Bodi pia ilipanga kuanza ujenzi wa jengo la ofisi Dodoma, kununua vifaa 30 kwa ajili ya kupimia ubora wa kazi za barabara zinazotekelezwa na Halmashauri nchini, kuhakiki takwimu za barabara nchini hususan barabara zilizo chini ya Halmashauri kwa lengo la kupata takwimu

sahihi za mtandao wa barabara na kufanya utafiti wa gharama za matengenezo ya barabara nchini kwa kushirikiana na kitengo cha *International Growth Center* kilichopo Benki Kuu ya Tanzania kwa lengo la kudhibiti gharama hizo ili kuleta ufanisi katika matumizi ya fedha za Mfuko. Vilevile, Bodi ilipanga kuendelea na ukaguzi wa kiufundi kwa kazi za matengenezo ya barabara ili kubaini kama kazi zilizofanyika zinalingana na thamani ya fedha za Mfuko zilizotumika (Value for Money).

116. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Bodi ya Mfuko ilikua imepokea kutoka Hazina jumla ya Shilingi 284,118,900,002. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi 178,231,000,002 ni makusanyo ya mwaka wa fedha 2014/15 na Shilingi 105,887,900,000 ni makusanyo ya mwaka wa fedha 2013/14. Bodi ilizigawa fedha hizo kwa Bodi yenyewe, TANROADS, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi. Aidha, Bodi imekwisha anza ujenzi wa jengo la ofisi Dodoma; utaratibu wa kununua vifaa vya kupimia ubora wa kazi unaendelea, utafiti wa maeneo mapya ya vyanzo vya mapato unaanza mwezi Juni 2015, ukaguzi wa kiufundi wa kazi za matengenezo ya barabara zinaendelea nchini na hadidu za rejea kwa kazi ya kuhakiki takwimu za barabara zimekamilika.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

117. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilipanga kusajili Wahandisi 800, Mafundi Sanifu 200 na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 25; kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi wahitimu 692; kukagua shughuli za kihandisi nchini na kukagua wa miradi ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri za Wilaya. Aidha, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilipanga kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri wote na kuendelea kusimamia viapo vya utii wa maadili ya taaluma zao.

118. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 966 na makampuni ya ushauri wa kihandisi 16 na kufikisha jumla ya wahandisi 15,062 waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali na makampuni ya ushauri wa kihandisi 279. Kati ya wahandisi waliosajiliwa 13,636 ni wazalendo na 1,426 ni wageni, makampuni ya ushauri wa kihandisi 201 ni ya kizalendo na 78 ni ya kigeni. Mafundi Sanifu (Engineering Technicians) 63 walisajiliwa. Aidha, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi viapo vya Utii wa Maadili ya Taaluma (Professional Oath) ambapo idadi ya wahandisi

1,909 walikula viapo. Aidha, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi wataalam 95, wahandisi washauri 24 na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 5 kwa kukiuka sheria ya usajili wa wahandisi.

Majukumu mengine yaliyotekelezwa na Bodi ni kuendelea kusimamia utekelezaji wa utaratibu wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote ili kuwafanya wahandisi kwenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia na hivyo kuwafanya wahandisi waendeleo kufanya shughuli zao za kihandisi kwa ufanisi. Wahandisi wataalam zaidi ya 3,250 walihudhuria mafunzo mbalimbali ya kujiendeleza. Bodi pia ilikagua miradi 193 ya ujenzi ili kuhakikisha kuwa inajengwa kwa ubora na inajengwa na wahandisi waliosajiliwa ambapo wahandisi wa kigeni 26 walibainika kufanya kazi bila usajili na kuchukuliwa hatua za kisheria. Kati yao 10 walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa na 16 walikataliwa usajili kwa sababu hawakuwa na sifa za kutosha na hivyo kurejeshwa makwao. Bodi vile vile iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu 781 ambapo kati yao wahandisi wahitimu 145 wa kike wanafadhiliwa na Serikali ya Norway. Jumla ya wahandisi wahitimu 2,892 wameshapitia kwenye Mpango huo tangu uanzishwe mwaka 2003. Aidha, Wahandisi

wahitimu zaidi ya 300 kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali za Serikali wameshahitimu mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi kama wahandisi wataalam.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

119. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili wataalam 60, ambapo Wabunifu Majengo ni 25 na Wakadiriaji Majenzi ni 35; kusajili Kampuni 24 za Wabunifu Majengo na Kampuni 10 za Wakadiriaji Majenzi na kuendelea kufanya ukaguzi wa shughuli za wataalamu kwenye miradi iliyopo nchini inayostahili kukaguliwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, Bodi iliendelea na mpango wa kuwajengea uwezo wahitimu katika fani ya Ubunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kukupitia mafunzo kwa vitendo na kuanzisha programu ya kutangaza na kuelimisha umma kuhusu shughuli za Bodi na umuhimu wa kushirikisha Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika kubuni nyumba za gharama nafuu.

120. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili Wabunifu Majengo 40 na Wakadiriaji Majenzi 43

na kufanya jumla ya Wabunifu Majengo waliosajiliwa hadi sasa kufikia 398 na Wakadiriaji Majenzi 294. Aidha, Bodi ilisajili Kampuni za Ubunifu Majengo 9 na Ukadiriaji Majenzi 8 na kufanya jumla ya Kampuni za Ubunifu Majengo zilizosajiliwa kufikia 327 na Ukadiriaji Majenzi 321. Vilevile, Bodi ilifanya ukaguzi wa shughuli za wataalam kwenye miradi katika mikoa 25 ya Tanzania Bara kama ifuatavyo: Dar es Salaam (870), Tanga (42), Pwani (81), Kigoma (30), Tabora (30), Dodoma (99), Singida (72), Mwanza (128), Mara (28), Shinyanga (50), Arusha (91), Kilimanjaro (26), Mbeya (30), Rukwa (16), Manyara (18), Ruvuma (11), Iringa (48), Morogoro (92), Simiyu (25), Kagera (50), Lindi (5), Mwanza (22), Njombe (14), Katavi (5) na Geita (21). Kazi nyingine zilizofanywa na Bodi ni kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu 42 katika fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na kutoa elimu kuhusu taaluma za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi kwa TAMISEMI na Askari Polisi katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Pwani, Morogoro, Singida, Tabora, Ruvuma, Njombe, Iringa, Katavi na Rukwa. Ili kujitangaza, Bodi ilitoa elimu kwa njia mbalimbali kuhusiana na majukumu ya Bodi na wajibu wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. Sambamba na hayo, Bodi iliendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa Sekondari kuhusiana na taaluma

ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi ambapo zawadi mbalimbali zilitolewa.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

121. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi 834 wa fani mbalimbali na kukagua miradi ya ujenzi 2,500. Bodi pia ilipanga kuendeleza Mfuko Maalum wa Kutoa Dhamana ya Kusaidia Makandarasi Wadogo na wa Kati (Contractors Assistance Fund) ili kuwajengea uwezo. Hadi kufikia Aprili, 2015 Bodi ilisajili Makandarasi wapya 936 wa fani mbalimbali na kusajili miradi 2,497 ambayo ina thamani ya kuanzia Shilingi milioni 10. Bodi pia ilikagua miradi 2,700 ya ujenzi, ambapo miradi 921 ilikutwa na kasoro. Makandarasi katika miradi yenye upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kusimamishwa kufanya kazi za ukandarasi na kufutiwa usajili. Aidha, Bodi iliendesha kozi za mafunzo 5 zenye lengo la kukuza uwezo wa makandarasi ambapo jumla ya makandarasi 212 walishiriki mafunzo hayo.

Baraza la Taifa la Ujenzi

122. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza la Taifa la Ujenzi lilipanga kutekeleza kazi zifuatazo: kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Ujenzi; kuandaa taarifa takwimu na majarida ya kiufundi kuhusu Sekta ya Ujenzi na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi, ukaguzi wa kiufundi na kiutaalam wa miradi yote ya ujenzi pamoja na utatuzi wa migogoro katika sekta ya ujenzi.

Baraza pia lilipanga kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 23 la ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na mwekezaji binafsi (Lindi Express Limited) lililoko barabara ya Samora, Dar es Salaam. Aidha, Baraza lilipanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya majengo ya kitega uchumi katika maeneo ya Regent Estate, Mbezi Beach jijini Dar es salaam na uendelezaji kiwanja kilichopo Dodoma.

Kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na mradi wa kukuza uwazi na uwajibikaji (Construction Sector Transparency Initiative (CoST)) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi, na kuendeleza jitihada za kukuza Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (Construction Industry Development Fund).

123. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Baraza la Taifa la Ujenzi lilitokeleza majukumu yafuatayo:

- (i) Baraza liliendesha mafunzo mbalimbali kwa wadau 81 wa sekta ya ujenzi. Kati ya hao walipatiwa mafunzo ya usimamizi na menejimenti ya mikataba ya ujenzi walikuwa (41), usuluhishi wa migogoro (28) na matengenezo na ukarabati wa majengo (12).
- (ii) Baraza linasimamia ujenzi wa jengo la kitega uchumi (Samora Tower) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90.
- (iii) Baraza lilishughulikia usuluhishi wa migogoro ya miradi ya ujenzi ipatayo 57. Aidha, Baraza limeendelea na utekelezaji wa majaribio wa mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji (transparency and accountability) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma ujulikanao kwa jina la “Construction Sector Transparency Initiative (CoST)”. Majaribio haya yanafadhiliwa na kuratibiwa katika ngazi ya kimataifa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID). CoST inatekelezwa kwa majaribio katika nchi saba yaani Ethiopia, Malawi, Philippines, Tanzania, Uingereza, Vietnam na Zambia.

- (iv) Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi (Technical Audit) wa miradi ipatayo 99 yenye thamani ya Shilingi bilioni 18.33. Miradi iliyokaguliwa inajumuisha miradi ya barabara 91 na miradi ya majengo 8. Ukaguzi huo ulibainisha upungufu ambapo Baraza lilitoa ushauri wa jinsi ya kuurekebisha.
- (v) Baraza lilifanya tafiti kuhusu: Upimaji wa tija na ubora wa kazi katika Sekta ya Ujenzi; Matatizo ya ushindani wa Makandarasi wazalendo katika kutekeleza miradi ya ujenzi ikilinganishwa na Makandarasi wa kigeni; Kanuni za mikataba katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kama vile barabara, na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa njia ya Kusanifu na Kujenga (Design and Build).

Vikosi vya Ujenzi (Corporation Sole Works Superintendent)

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/15, Vikosi vya Ujenzi vilipanga kufanya ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi pamoja na nyumba za Viongozi wa Serikali, ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Msangamkuu Mtwara, pamoja na kufanya

ukarabati wa ofisi na maghala ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – Dar es Salaam.

Kazi nyingine ni kufanya ukarabati wa karakana za Vikosi vya Ujenzi Dar es Salaam na Dodoma pamoja na kuanzisha mradi wa utengenezaji na uuzaji wa vifaa vya ujenzi ‘Building Materials Centres’ Dar es Salaam na Dodoma

125. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Vikosi vya Ujenzi vilitekeleza miradi inayohusu ujenzi wa vituo vya abiria kwa ajili ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, ujenzi wa nyumba ya makazi ya Jaji eneo la Bugando Mwanza, ujenzi wa nyumba ya makazi ya Idara ya uhamiaji jijini Mwanza, pamoja na ukarabati wa madaraja katika barabara ya Manchali – Mbande – Kongwa – Dodoma.

Vikosi vya ujenzi vilifanya pia ukarabati katika majengo ya Ofisi za Mameneja wa TANROADS mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, ujenzi wa soko la mboga na matunda Michungwani Muheza na ujenzi wa jengo la ofisi (Kero office) wilayani Rombo. Aidha, Vikosi vya Ujenzi vimeendelea na utekelezaji wa mradi wa utengenezaji wa vifaa

vya ujenzi (blocks and pre-cast concrete elements) jijini Dar es Salaam.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

126. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Kituo kilipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji hapa nchini kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Morgan (Morgan State University) cha Marekani.
- ii) Kuandaa warsha na kozi zinazolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.
- iii) Kuendelea kutoa huduma za maktaba ya Kituo kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kuboresha njia za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji habari.
- iv) Kushiriki katika Kamati ya Kujenga Uwezo ya SADC (Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee) kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi.

127. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Kituo kilitokeleza kazi zifuatazo:

- i) Kituo kilishiriki katika mikutano 2 ya kimataifa na mikutano 3 ya ndani ya nchi inayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.
- ii) Kituo kimeshiriki katika Mradi unaotekelezwa na Umoja wa Mamlaka za Barabara katika nchi za SADC (*Association of Southern African National Road Agencies* – ASANRA) unaolenga kutambua mapungufu ya ujuzi na hivyo kutoa mapendekezo ya kujenga uwezo kwa watendaji wa Mamlaka za Barabara.
- iii) Kituo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Morgan (Morgan State University) cha Marekani kimeandaa pendekezo la kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto za msongamano wa magari katika miji mbalimbali hapa nchini kwa kuanzia na Jiji la Dar es Salaam. Pendekezo la kufanya utafiti limewasilishwa COSTECH kwa hatua zaidi na idhini ya kutengewa fedha za utekelezaji.

- iv) Tanzania kupitia Kituo cha TanT² iliendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kujenga uwezo ya SADC kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi.

Chuo cha Ujenzi Morogoro

128. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Ujenzi cha Morogoro katika mwaka wa fedha 2014/15, kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi 1,060 katika fani za ufundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na udereva. Aidha, Chuo kilipanga kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la madarasa na maabara ya vifaa vya ujenzi.

Hadi kufikia Aprili, 2015 jumla ya wanafunzi wa fani za ujenzi **637** walipata mafunzo chuoni kama ifuatavyo: Basic Artisans Course 390, Basic Driving Course 141, Passenger Service Vehicle (PSV) Driving Course 53 na Technician Maintenance Management Course 53.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI)

129. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Chuo kilipanga kuendelea kutoa mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na kuhamasisha matumizi ya

teknolojia hii hapa nchini na nje ya nchi, kushiriki katika makongamano na maonyesho mbalimbali ya uhamasishaji ndani na nje ya nchi ili kutoa elimu juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, Chuo kilipanga kutoa mafunzo na uhamasishaji kwa lengo la kuwajengea uwezo wakufunzi na watumishi wa kada mbalimbali.

130. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Chuo kilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wananchi 312 katika Halmashauri za Wilaya ya Busokelo na Rungwe. Pamoja na mafunzo hayo, wananchi hao walipata ajira.
- (ii) Kuwajengea uwezo na kuwaendeleza kitaaluma watumishi wa Chuo.
- (iii) Mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi yalitolewa kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya.

D. MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Makadirio ya Mapato

131. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **47,765,000.00** katika mwaka wa fedha 2015/16, kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Ufundi na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi.

Matumizi ya Kawaida

132. **Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16 ni Shilingi **42,142,581,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **36,778,993,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **5,363,588,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

133. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi 890,572,770,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ambayo ni ya kimkakati (Strategic) na Miradi isiyo ya kimkakati (Non-Strategic). Kati ya fedha hizo **Shilingi**

198,360,000,000.00 ni fedha za ndani, **Shilingi 85,572,770,000.00** ni fedha za nje na **Shilingi 606,640,000,000.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara.

Miradi ya Maendeleo ambayo ni ya kimkakati inahusu ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na vivuko ambapo kiasi cha **Shilingi 278,382,770,000.00** kimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 193,360,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 85,022,770,000.00** ni fedha za nje.

Miradi isiyo ya kimkakati ni pamoja na Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali, Usalama Barabarani, Mazingira na Kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara. Katika mwaka wa fedha 2015/16, miradi hiyo imetengewa jumla ya **Shilingi 5,550,000,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 550,000,000.00** ni fedha za nje.

Vipaumbele vya miradi itakayotekelezwa ni katika miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na wahisani na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/16, ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.1**. Aidha, maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo: –

MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI

Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko Shilingi Milioni 2,774.118

134. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu una lengo la kujenga maegesho (Landing Ramps) ili vivuko viweze kuegeschwa na kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko kwa urahisi na usalama. Katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa Shilingi milioni **2,774.118** kwa ajili ya kazi za ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo (Shilingi milioni 1,414.710), ujenzi wa majengo ya abiria kwa kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo (Shilingi milioni 120.750), upanuzi wa eneo la maegesho katika kivuko cha Kigamboni (Shilingi milioni 72.450) pamoja na ukarabati wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni (Shilingi milioni 120.750).

135. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa maegesho ya Msangamkuu – Msemo (Shilingi milioni 36.220), Iramba – Majita (Shilingi milioni 72.450), Ilagala – Kajeje (Shilingi milioni 60.370), Kilombero upande wa Ulanga (Shilingi milioni 28.980), Bugolora upande wa Ukara (Shilingi milioni 44.670) pamoja na Kahunda – Maisome (Shilingi milioni 242.460). Aidha, fedha hizi zitatumika

katika ukarabati wa maegesho ya kivuko cha Pangani (Shilingi milioni 48.300), ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumachelli (Shilingi milioni 79.690), ujenzi wa maegesho katika vituo viwili kwa usafiri wa majini Jijini Mwanza (Shilingi milioni 205.270) pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria kwa usafiri wa majini jijini Mwanza (Shilingi milioni 48.30). Usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hii umetengewa Shilingi milioni 178.750 .

Ununuzi wa Vivuko Vipya Shilingi Milioni 2,036.620

136. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa Shilingi milioni **2,036.620** kwa ajili ya kazi zifuatazo: ununuzi wa kivuko kipya kitakachofanya kazi kati ya Magogoni – Kigamboni (Shilingi milioni 507.150), ununuzi wa kivuko kitakachofanya kazi kati ya Kigongo – Busisi (Shilingi milioni 852.990), ununuzi wa mashine za kisasa za kukatia tiketi (ticket vending machines) kwa ajili ya vivuko vya Kisorya, Ilagala na Pangani (Shilingi milioni 144.900) pamoja na kuboresha mashine za kukatia tiketi kwa kivuko cha Magogoni – Kigamboni (Shilingi milioni 241.500)

137. **Mheshimiwa Spika**, kazi zingine ni ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA

(Shilingi milioni 144.900) pamoja na maandalizi ya sera kuhusu Usimamizi wa Magari ya Serikali (Shilingi milioni 48.300). Kiasi cha Shilingi milioni 98.880 kimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi hii.

Ukarabati wa Vivuko Shilingi Milioni 661.350

138. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni **661.350** kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV Mwanza (Shilingi milioni 120.750), MV Magogoni (Shilingi milioni 178.710) pamoja na MV Geita (Shilingi milioni 88.140). Kazi nyingine ni ukarabati wa kivuko cha MV Kome I (Shilingi milioni 108.670), MV Nyerere (Shilingi milioni 48.300) na MV Pangani II (Shilingi milioni 84.520). Kiasi cha Shilingi milioni 32.258 kimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi hii.

Ujenzi na Ukarakati wa Nyumba na Majengo ya Serikali Shilingi Milioni 2,689.463

139. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kujenga nyumba kwa ajili ya ofisi za Serikali na makazi ya Viongozi na Watumishi wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shilingi milioni 200.000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo na Shilingi milioni

655.090 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mikoa ya Shinyanga (1), Kagera (1), Mtwara (1), Kilimanjaro (1) na Dar es Salaam (1). Aidha, Shilingi milioni 111.000 zimetengwa kwa ajili ya usanifu na maandalizi ya michoro ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha pamoja cha mpaka wa Tunduma (Tunduma One Stop Border Post).

140. **Mheshimiwa Spika**, Shilingi milioni 126.000 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi (awamu ya nne), Shilingi milioni 100.000 zimetengwa kwa ajili ya usanifu na maandalizi ya michoro ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara ya Ujenzi na Shilingi milioni 100.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio na kuweka mfumo wa ulinzi katika nyumba za viongozi wa Serikali zilizopo Mikocheni, Kijitonyama na Msasani Peninsular. Aidha, Shilingi milioni 564.250 zitatumika kufanyia matengenezo na ukarabati wa nyumba za viongozi wa Serikali, na Shilingi milioni 234.000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa samani kwenye Ikulu ndogo katika mikoa mbalimbali na kwa viongozi wa Wizara ya Ujenzi wenye stahili ya kupewa samani.

141. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 150.000 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa

Karakana za Serikali chini ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na Dodoma. Shilingi milioni 40.000 zimetengwa kwa ajili ya kufanya maboresho ya kiutendaji kwa kufanya ukarabati wa karakana za Vikosi vya Ujenzi (Carpentry Workshops) zilizopo Dar es Salaam na Dodoma. Jumla ya Shilingi milioni 259.123 zimetengwa kwa ajili ya kulipia gharama za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi milioni 150.000 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2015/16, kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwaongezea ujuzi wataalam wazalendo.

MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

**BARABARA YA DAR ES SALAAM – CHALINZE
– MOROGORO EXPRESSWAY (KM 200)
SEHEMU YA DAR ES SALAAM – CHALINZE
(KM 100) – SHILINGI MILIONI 2,450.000**

143. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi ni kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100) kwa kiwango cha “Expressway”. Mshauri Mwelekezi (Transaction

Advisor) amekwishapatikana na upembuzi yakinifu na utayarishaji wa nyaraka za zabuni unaendelea. Mradi huu utatekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi “Public Private Partnership” (PPP).

144. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/2016, kiasi cha Shilingi milioni 1,450.000 kimetengwa kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100). Aidha, Shilingi milioni 1,000.000 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24).

BARABARA YA WAZO HILL – BAGAMOYO – MSATA NA BAGAMOYO – SAADANI – TANGA (KM 178) – SHILINGI MILIONI 4,410.000

145. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Bagamoyo – Makofia – Msata (km 64). Aidha, lengo la mradi huu ni kukamilisha usanifu wa kina kwa barabara ya Bagamoyo – Saadan – Tanga (km 178). Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 4,230.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata. Pia kiasi cha Shilingi milioni 180.000

kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina wa barabara ya Bagamoyo – Saadani – Tanga.

BARABARA YA USAGARA – GEITA – KYAMYORWA (KM 422) SEHEMU YA UYOVU – BIHARAMULO (KM 112) – SHILINGI MILIONI 4,970.000

146. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Uyovu – Biharamulo (km 112) pamoja na kukarabati barabara ya Kyamyorwa – Geita (km 220) na barabara ya Geita – Usagara (km 90).

147. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 4,241.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Bwanga - Biharamulo (km 112), kiasi cha Shilingi milioni 324.000 kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo (km120) na kiasi cha Shilingi milioni 405.000 kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi kwa sehemu ya Geita – Usagara (km 90).

**BARABARA YA KIGOMA – KIDAHWE – UVINZA
– KALIUA – TABORA (KM 504.70)–SHILINGI
MILIONI 11,298.915**

148. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara kati ya Kigoma na Tabora (km 443). Kazi ya ujenzi ujenzi wa daraja la Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (km 48) ilikamilika Novemba, 2013. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Uvinza (km 76.6) umekamilika Oktoba, 2013 na kwa barabara ya Tabora – Ndoni (km 42) ujenzi umekamilika Januari, 2014. Kazi ya ujenzi kwa barabara ya Ndoni – Urambo (km 52) inaendelea. Aidha, ujenzi wa barabara ya Kaliua – Kazilambwa (km 56) nao unaendelea. Maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Uvinza – Malagarasi (km 51.10), Urambo – Kaliua (km 33) na Kazilambwa – Chagu (km 40) yanaendelea.

149. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 867.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 1,108.915 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho (final account) ya mkandarasi wa Daraja la Malagarasi. Kiasi cha Shilingi milioni 864.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mkandarasi wa barabara ya Kidahwe – Uvinza (km 76.6). Kiasi cha Shilingi milioni

2,771.000 kimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mkandarasi wa barabara ya Tabora – Ndonno (km 42), Shilingi milioni 2,913.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Ndonno – Urambo (km 52) na kiasi cha Shilingi milioni 2,370.000 kimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Urambo - Kaliua - Ilunde – Uvinza (km 56). Kwa upande wa barabara ya Uvinza – Malagarasi (km 51) zimetengwa Shilingi milioni 405.000.

BARABARA YA MARANGU – TARAKEA – KAMWANGA/BOMANG’OMBE – SANYA JUU (KM 173), ARUSHA – MOSHI – HOLILI (KM 140), MARANGU – ROMBO MKUU NA KILACHA – MWIKA (KM 32), KIA – MERERANI (KM 26), KWA SADALA – MASAMA – MACHAME JUNCTION (KM 16.0) NA KIBOROLONI – KIHARARA – TSUDUNI – KIDIA (KM 10.8) – SHILINGI MILIONI 12,010.636

150. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 96) na Sanya Juu – Kamwanga (km 75) kwa kiwango cha lami na kukarabati barabara ya Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha Bypass (km 140). Ujenzi huo utachoea ukuaji wa sekta ya utalii kuzunguka mlima Kilimanjaro na hivyo kukuza uchumi wa nchi. Ujenzi wa sehemu ya Tarakea

– Rongai – Kamwanga (km 32) ulikamilika Septemba, 2009, na ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) ulikamilika Januari, 2011. Kazi za ujenzi wa sehemu ya Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32) zilikamilika Machi, 2013. Aidha, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu za KIA – Mererani (km 26), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16.0) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) zinaendelea.

151. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 198.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Tarakea – Rombo na Shilingi milioni 464.000 kwa ajili ya barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Mwika – Kilacha (km 32). Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 2,026.000 kimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Kamwanga (km 75). Jumla ya Shilingi milioni 934.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 6,160.636 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa kwa mradi wa Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.10) na njia mbili kwa sehemu ya Arusha Bypass (km 42.41). Aidha, Shilingi 1,013.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani (km 26), Shilingi

milioni 405.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Machame Jct (km 16) na kiasi cha Shilingi milioni 810.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.80).

NANGURUKURU – MBWEMKURU (KM 95) – SHILINGI MILIONI 810.000

152. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo ambayo ni kiungo muhimu kati ya Dar es Salaam na mikoa ya Kusini. Ujenzi wa barabara hii ulikamilika Januari, 2008. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 810.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho (final account) ya mkandarasi.

DODOMA – MANYONI (KM 127) – SHILINGI MILIONI 1,015.000

153. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design & Build). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na ulikamilika mwezi Novemba, 2009. Vilevile, mradi huu unahusisha kuanza ujenzi kwa

kiwango cha lami barabara ya mchepuo wa kuingia Manyoni mjini (km 4.8). Aidha, katika kupunguza vizuizi ambavyo sio vya kiushuru kwa magari yaendayo nchi za nje na kupunguza msongamano kwenye mizani, maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi cha Muhalala (Manyoni) “One Stop Inspection Station – OSIS”.

154. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 531.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (km 4.8) na malipo ya gharama za usuluhishi (arbitration) kwa sehemu ya Dodoma – Manyoni (km 127). Aidha, Shilingi milioni 484.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa *Muhalala One Stop Inspection Station* (OSIS).

MBWEMKURU – MINGOYO (KM 95) – SHILINGI MILIONI 217.000

155. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu umehusisha kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbwemkuru – Mingoyo yenye urefu wa kilometa 95 kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (*Design & Build*). Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo

na ujenzi wake ulikamilika Desemba, 2007. Katika bajeti ya mwaka 2015/16, barabara hii imetengewa kiasi cha Shilingi milioni 217.000 fedha za ndani kwa ajili ya malipo ya mkandarasi.

PORT ACCESS ROAD (NELSON MANDELA ROAD) REHABILITATION (KM16.8) – SHILINGI MILIONI 967.000

156. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu lilikuwa ni kukarabati na kuimarisha barabara ya Nelson Mandela (km15.6) iliyokuwa imeharibika ili kurahisisha usafiri wa magari ya mizigo yanayotoka na kuingia Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 725.000 fedha za ndani kwa ajili ya malipo ya mkandarasi. Aidha, Shilingi milioni 242.000 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Nelson Mandela sehemu ya Dar Port – TAZARA (km 6) kuwa njia sita.

BARABARA YA DUMILA – KILOSA (KM 63) – SHILINGI MILIONI 3,363.000

157. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Dumila – Kilosa (km 63). Kazi ya ujenzi

wa barabara ya Dumila – Rudewa (km 45) imekamilika Desemba, 2013. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, barabara ya Dumila – Kilosa (km 63) imetengewa Shilingi milioni 3,121.000 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 18). Aidha, Shilingi 242.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa mizani eneo la Dumila.

BARABARA YA SUMBAWANGA – MATAI – KASANGA PORT (KM 112) – SHILINGI MILIONI 4,633.000

158. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km. 112) kwa kiwango cha lami. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na unatekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga. Kazi za ujenzi zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2015/16, barabara hii imetengewa kiasi cha Shilingi milioni 4,150.000 kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi. Aidha, Shilingi milioni 483.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

**UJENZI WA MADARAJA YA KIRUMI,
NANGOO, SIBITI, KILOMBERO, KAVUU,
MBUTU, RUHEKEI, RUHUHU, MOMBA,
SIMIYU, WAMI, LUKULEDI II, SELANDER NA
UNUNUZI WA EMERGENCY BRIDGE PARTS:
SHILINGI MILIONI 9,587.000**

159. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi – Maligisu, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge, Daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga, Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga – Manonga, Daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbinga – Mbamba Bay, Daraja la Ruhuhu kwenye barabara ya Kitai – Lituhi, Daraja la Momba kwenye barabara ya Sitalike – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo (Rukwa/Mbeya Border), Daraja la Simiyu kwenye barabara Mwanza – Musoma, Daraja la Wami barabara ya Chalinze – Segera, Daraja la Lukuledi II kwenye barabara Mtama – Kitangali – Newala, ujenzi wa daraja jipya la Selander na kununua *Emergency Bridge Parts*.

160. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 608.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya Ukarabati wa Daraja la Kirumi, Daraja la Nangoo limetengewa Shilingi milioni 203.00, Daraja la Sibiti Shilingi milioni 1,216.000, Daraja la Kilombero Shilingi milioni 3,039.000, Daraja la Kavuu limetengewa Shilingi milioni 405.000, Daraja la Mbutu Shilingi milioni 1,402.00, Daraja la Ruhekei Shilingi milioni 101.000, Daraja la Momba Shilingi milioni 810.000. Daraja la Simiyu Shilingi milioni 527.000, Daraja Jipya la Wami (New Wami Bridge) Shilingi milioni 81.000, Daraja la Lukuledi II Shilingi milioni 405.000 na Daraja la Sukuma Shilingi milioni 81.000. Aidha, Shilingi milioni 425.000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa Emergency Bridge Parts, Shilingi milioni 203.000 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Ruhuhu na Shilingi milioni 81.000 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa daraja jipya la Selander.

BARABARA YA NEW BAGAMOYO (KAWAWA JCT – TEGETA KM 17.1) – SHILINGI MILIONI 1,013.000

161. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kupanua barabara hii kutoka njia mbili za sasa hadi njia nne kuanzia makutano ya barabara za Kawawa na Ali Hassan Mwinyi eneo

la Morocco hadi Tegeta ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 12.9) ambayo imekamilika Julai, 2014. Kwa sasa iko kwenye kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu na awamu ya pili ni sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,013.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuhamisha miundombinu kwenye eneo la ujenzi (mabomba ya maji, nguzo na nyaya za umeme/simu n.k) sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

BARABARA YA KYAKA – BUGENE – KASULO (KM 178) – SHILINGI MILIONI 2,446.000

163. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi ni kujenga barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (sehemu ya Kyaka – Bugene) yenye urefu wa kilometa 59.1 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,446.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**BARABARA YA ISAKA – LUSAHUNGA (KM 242)
NA LUSAHUNGA – RUSUMO NA NYAKASANZA –
KOBORO (KM 150)– SHILINGI MILIONI
8,766.000**

164. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Isaka – Lusahunga yenye urefu wa kilometa 242 kwa kiwango cha lami. Mradi wa ukarabati unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili (2) ili kuharakisha utekelezaji: Isaka – Ushirombo (km 132) na Ushirombo – Lusahunga (km 110). Kwa sehemu ya Isaka – Ushirombo, kazi zimekamilika Novemba, 2013. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga zinaendelea.

165. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, barabara ya Isaka – Ushirombo imetengewa fedha za ndani Shilingi milioni 4,665.000 kwa ajili ya malipo ya mkandarasi na Shilingi milioni 3,650.000 fedha za ndani kwa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga kwa ajili ya kuendelea na ukarabati. Kiasi cha Shilingi milioni 209.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero. Aidha, Shilingi 242.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa

mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo ya *Mwendakulima Weigh in Motion*–WIM).

**BARABARA YA MANYONI – ITIGI – TABORA
(KM 264) – SHILINGI MILIONI 8,711.000**

166. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora kwa kuanzia sehemu ya Manyoni – Chaya yenye urefu wa kilometa 89.35, sehemu ya Tabora – Nyahua yenye urefu wa kilometa 85 kwa kutumia fedha za ndani. Kazi za ujenzi zinaendelea kwa sehemu zote mbili. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Nyahua – Chaya (km 90) yanaendelea.

167. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 4,052.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Tabora – Nyahua na Shilingi milioni 4,173.000 kwa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya. Kwa upande wa barabara ya Nyahua – Chaya (km 85.4) kiasi cha Shilingi milioni 486.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu hii ya barabara kwa kiwango cha lami.

BARABARA YA KOROGWE – HANDENI (Km 65) – SHILINGI MILIONI 2,576.000

168. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Korogwe – Handeni (km 65). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zimekamilika Novemba 2013. Katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 2,576.000 kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi.

BARABARA ZA MIKOA SHILINGI MILIONI 12,391.116

169. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuzifanyia ukarabati barabara za Mikoa kwa kiwango cha changarawe, kujenga kwa kiwango cha lami na kujenga madaraja katika baadhi ya barabara za mikoa yote ya Tanzania Bara.

170. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa upande wa barabara za mikoa ni ukarabati wa jumla ya kilometa **746.5** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **60.3** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **17** utafanyika. Kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zitafanyika katika Mikoa yote ya

Tanzania Bara. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo imeonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**BARABARA YA MWANZA/SHINYANGA
BORDER – MWANZA (KM 10) SHILINGI
MILIONI 20.000**

171. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kuendelea na kufanya ukarabati wa sehemu zilizoharibika katika barabara hii. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 20.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati.

**BARABARA YA HANDENI – MKATA (KM 54) –
SHILINGI MILIONI 1,817.000**

172. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni – Mkata (km 54). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi wa barabara hii zilikamilika. Katika mwaka 2015/16, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 1,817.000 kwa ajili ya malipo ya mkandarasi.

BARABARA YA MWANDIGA – MANYOVU (KM 60) – SHILINGI MILIONI 6.000

173. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi ni kujenga barabara ya kutoka Mwandiga hadi Manyovu inayounganisha Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa barabara hii ulikamilika Oktoba, 2010. Katika mwaka 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 6.000 kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho (final account) ya mkandarasi.

DARAJA LA UMOJA – SHILINGI MILIONI 157.000

174. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu lilikuwa ni kujenga Daraja katika mto Ruvuma eneo la Mtambaswala/Negomane ili kuunganisha nchi za Tanzania na Msumbiji. Daraja hili lilijengwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (Design and Build). Mradi huu uligharamiwa na Serikali za Tanzania na Msumbiji na ulikamilika mwezi Mei, 2010. Katika mwaka 2015/16, daraja hili limetengewa Shilingi milioni 157.000 kwa ajili ya malipo ya mwisho (final account) ya mkandarasi.

**BARABARA ZA KUONDOA MSONGAMANO
KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM (KM109.35)
SHILINGI MILIONI 12,044.000**

175. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi na ukarabati wa barabara za Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Barabara hizo ni: Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga jct (km 2.7) kazi za ujenzi zinaendelea; ujenzi wa barabara ya Jet Corner – Vituka – Devis (km 10.3) umekamilika Septemba, 2013; sehemu ya Ubungo Maziwa – External kazi za ujenzi zimekamilika na awamu ya pili ni kuendelea na ujenzi sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.6); kuanza ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule – External (km 9.00), Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Tegeta – Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi (Morogoro Road) (km 20), Tangi Bovu – Goba (km 9.00), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.60), Kibamba – Kisopwa (sehemu ya Kibamba – Mlonganzila, (km 4.0), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) (sehemu ya Kitunda – Moshi Bar (km 3.2) na kuanza ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo (km 4.00). Aidha, mradi wa mabasi yaendayo haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure) na vituo vyake unaendelea.

176. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 245.000 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobakia kwa barabara ya Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga jct, Shilingi milioni 73.000 kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa barabara ya Ubungo Terminal – Kigogo R/About, Shilingi milioni 523.000 kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa barabara ya Jet Corner – Vituka – Devis Corner, Shilingi milioni 1,013.000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo, Shilingi milioni 2,026.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kimara – Kilungule – External, Shilingi milioni 2,431.000 kwa ajili ya barabara ya Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana, Shilingi milioni 2,026.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tegeta – Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi (Morogoro Road), Shilingi milioni 1,216.000 kwa ajili ya barabara ya Tangi Bovu – Goba, Shilingi milioni 608.000 kwa ajili ya barabara ya Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni na Shilingi milioni 608.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kibamba – Kisopwa (sehemu ya Kibamba – Mlonganzila – km 4.0).

177. **Mheshimiwa Spika**, Shilingi milioni 405.000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) sehemu ya Kitunda – Moshi Bar (km 3.2), Shilingi milioni 608.000 kwa ajili ya barabara ya Ardhi – Makongo na Shilingi 242.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Maji Chumvi – Chang’ombe – Barakuda – (km 2.5). Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 20.000 zitatumika kufuatilia na kusimamia ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure).

**BARABARA YA NDUNDU – SOMANGA (KM 60)
– SHILINGI MILIONI 3,598.260**

178. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika Februari, 2015. Mradi huu wa barabara (km 60) ulifadhiliwa kwa pamoja na Kuwait Fund, OPEC Fund na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 1,278.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 1,774.260 fedha za nje kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa mradi wa barabara hii. Aidha, Shilingi milioni 546.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa Daraja la Mkapa.

**KIDATU – IFAKARA – LUPILO – MALINYI –
LONDO – LUMECHA/SONGEA (KM 396)
SHILINGI MILIONI 533.851**

179. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kidatu hadi Lumecha/Songea chini ya msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na mchango wa Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 41.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 492.851 fedha za nje kwa ajili ya Mhandisi Mshauri anayefanya kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara hii.

**BARABARA YA TABORA – IPOLE – KOGA –
MPANDA (KM 359) – SHILINGI MILIONI
2,941.000**

180. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mpanda – Koga – Ipole (km 260) na Tabora – Sikonge – Ipole (km 99) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,037.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mpanda – Koga – Ipole (km 260) na Shilingi milioni 1,904.000 kwa ajili ya sehemu ya Tabora – Sikonge – Ipole (km 99).

BARABARA YA MAKUTANO – NATTA – MUGUMU/ LOLIONDO – MTO WA MBU (KM 452) – SHILINGI MILIONI 3,897.000

181. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta – Mugumu (km 125) sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) unaendelea. Aidha, kazi ya usanifu wa kina wa barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo (km 213) ilikamilika mwaka 2011.

182. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,276.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) na Shilingi milioni 1,621.000 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mto wa Mbu – Loliondo (km 213).

BARABARA YA IBANDA – ITUNGI/KIWIRA PORT (KM 26) – SHILINGI MILIONI 405.000

183. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara ya Ibanda – Itungi/Kajunjumele Kiwira Port (km 26) kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni kiungo muhimu kwa bandari ya Itungi/Kiwira. Katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha

Shilingi milioni 405.000 fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya Ibanda – Itungi/Kiwira Port sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port yenye urefu wa kilometa 5.6.

BARABARA YA TANGA – HOROHORO (KM 65) – SHILINGI MILIONI 53.000

184. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Tanga – Horohoro (km 65) na mradi huu ulikamilika mwezi Oktoba, 2012. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 53.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya fidia.

BARABARA YA NZEGA – TABORA (KM 114.7) – SHILINGI MILIONI 5,336.000

185. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Nzega – Tabora (km 114.7) kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili za Nzega – Puge (km 58.6) ambao ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea na Puge – Tabora (km 56.10) ambao ujenzi umekamilika.

186. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,713.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na

ujenzi wa sehemu ya Nzega – Puge na Shilingi milioni 2,623.000 kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa sehemu ya Puge – Tabora.

BARABARA YA SUMBAWANGA – MPANDA – KIDAHWE (KM 438) – SHILINGI MILIONI 11,692.000

187. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi ni kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kidahwe (km 438) kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi kwa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kizi – Sitalike – Mpanda (km 95) na Mpanda – Mishamo (km 100) zinaendelea.

188. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 3,586.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga–Kanazi, Shilingi milioni 3,586.000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kanazi – Kizi – Kibaoni na Shilingi milioni 2,681.000 kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Kizi – Sitalike – Mpanda. Kiasi cha Shilingi milioni 1,839.000 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Mishamo (100km).

BARABARA YA NYANGUGE – MUSOMA (KM 183) NA MCHEPUO WA USAGARA – KISESA (KM 17) NA BULAMBA – KISORYA (KM 51): SHILINGI MILIONI 8,957.000

189. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kukarabati barabara ya Nyanguge hadi Musoma (km 183), kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 17 za mchepuo wa barabara ya Usagara – Kisesa na Bulamba – Kisorya(km 51). Ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu (km 80) kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza, ujenzi wa kilometa 17 za mchepuo wa barabara ya Usagara – Kisesa unaendelea na ujenzi kwa sehemu ya Bulamba – Kisorya (km 51) unaendelea. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) ulikamilika mwezi Novemba, 2014. Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nyamuswa – Bunda yenye urefu wa kilometa 24.5 unaendelea pia.

190. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 1,013.000 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu (km 80). Kiasi cha Shilingi milioni 2,932.000 kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi kwa mradi wa Simiyu /Mara Border – Musoma (km 85.5). Kiasi cha Shilingi milioni 1,621.000

kimetengwa kwa sehemu ya barabara ya Kisesa – Usagara Bypass kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 1,823.000 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa sehemu ya Kisorya – Bunda (km 51), kiasi cha Shilingi milioni 405.000 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Nyamuswa – Bunda (km 24.5), Shilingi milioni 1,163.000 zimetengwa kwa ajili ya malipo yagharama za usuluhishi (arbitration) kwa mradi wa barabara za Mwanza Mjini (Mwanza Transport Project).

BARABARA YA MAGOLE – MZIHA (MAGOLE – TURIANI KM 48.8) – SHILINGI MILIONI 2,495.000

191. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Magole – Mziha (km 115), sehemu ya Magole – Turiani yenye urefu wa kilometa 48.8 kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi wa barabara hii inaendelea. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,495.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Magole – Turiani (km 48.8).

UJENZI WA FLYOVERS DSM NA KUBOresha MAKUTANO YA BARABARA – SHILINGI MILIONI 12,473.231

192. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga barabara za juu (Flyover) eneno la TAZARA ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwenye makutano ya barabara za Mandela na Nyerere. Kuanza kujenga kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design and Build) barabara za juu na kuboresha makutano (Flyover & Intersections) ya Chang'ombe, Ubungo, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata na Morocco katika jiji la Dar es Salaam. Aidha maandalizi ya upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA kuwa njia 6 (6 lanes) yanaendelea.

193. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 619.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 9,980.231 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa 'Flyover' ya TAZARA. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 900.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kabla ya kuanza ujenzi wa "Interchange" ya Ubungo. Shilingi milioni 732.000 zimetengwa kwa ajili ya maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco, Shilingi milioni 242.000 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi

wa barabara ya TAZARA – JNIA (km 6) kuwa njia 6 (6 lanes).

BARABARA YA MWIGUMBI – MASWA – BARIADI – LAMADI (KM 171.8) (BARIADI – LAMADI – KM 71.8) – SHILINGI MILIONI 4,247.000

194. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi yenye jumla ya kilometa 171 kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) zinaendelea. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi (km 100) yamekamilika.

195. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 2,424.000 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) na kiasi cha Shilingi milioni 1,823.000 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50).

**BARABARA YA TABORA – IPOLE – RUNGWA
(IPOLE–RUNGWA – KM 173.2) – SHILINGI
MILIONI 504.000**

196. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami sehemu ya Ipole – Rungwa yenye urefu wa kilometa 50 kutoka Ipole. Upembuzi yakinifu na usanifu unaendelea. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 504.000 kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**BARABARA YA KIDAHWE – KASULU –
KIBONDO – NYAKANAZI (KM 310) – SHILINGI
MILIONI 7,086.000**

197. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi – (km 310) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu kama ifuatavyo: Sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50) na Nyakanazi – Kibondo (Km 50) ujenzi unaendelea. Aidha, maandalizi ya usanifu yanaendelea kwa sehemu iliyobaki ya Nyakanazi – Kasulu/Manyovu (km 250).

198. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 3,526.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na

ujenzi wa kilometa 50 sehemu ya Kidahwe – Kasulu, Shilingi milioni 3,526.000 kwa ajili ya sehemu ya Nyakanazi – Kibondo (km 50). Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 34.000 kimetengwa kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina sehemu iliyobaki ya Nyakanazi – Kasulu/Manyovu (km 250).

BARABARA YA KWENDA UWANJA WA NDEGE WA MAFIA (MAFIA AIRPORT ACCESS ROAD, KM 14) – SHILINGI MILIONI 1,001.000

199. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo kuingia Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Access Road) ili kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa na Shirika la Misaada la Marekani (MCC) ambalo limetoa fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia kwa makubaliano na Serikali ya Tanzania kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami imekamilika mwezi Januari, 2015. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,001.000 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi.

DODOMA UNIVERSITY ROAD (KM 12) – SHILINGI MILIONI 1,216.000

200. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara

ya Chuo Kikuu cha Dodoma yenye urefu wa kilometa 12. Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami inaendelea. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,216.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

DARAJA LA KIGAMBONI NA BARABARA YA MAINGILIO YA DARAJA – SHILINGI MILIONI 2,215.000

201. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi ni kujenga daraja litakalounganisha Jiji la Dar es Salaam na mji wa Kigamboni ikiwa ni pamoja na barabara ya maingilio ya Kigamboni – Vijibweni yenye urefu wa kilometa 10.

202. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,006.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa daraja, na Shilingi milioni 209.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya maingilio ya Mjimwema – Vijibweni (km 10). Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na NSSF ambapo Serikali inachangia asilimia 40 na NSSF wanachangia asilimia 60.

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA SHILINGI MILIONI 606,640.000

203. *Mheshimiwa Spika*, fedha hizi ni kwa ajii ya matengenezo na ukarabati wa barabara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira na kazi zinazohusika na ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara.

UJENZI WA NJIA ZA MAGARI MAZITO NA MAEGESHO YA DHARURA KWA AJILI YA KUIMARISHA BARABARA KATIKA UKANDA WA KATI (PROVIDING LANE ENHANCEMENT INCLUDING CLIMBING LANES, PASSING BAYS, REST AND EMERGENCY LAY BAYS ON CENTRAL CORRIDOR) – SHILINGI MILIONI 81.000

204. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga njia za magari mazito na maegesho ya dharura kwa ajili ya kuimarisha barabara katika ukanda wa kati (providing lane enhancement including climbing lanes, passing bays, rest and emergency lay bays on central corridor). Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 81.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa maeneo ya kujenga.

UPANUZI WA BARABARA YA JNIA – PUGU (KM 8.0) KUWA NJIA SITA – SHILINGI MILIONI 242.000

205. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kupanua barabara ya Pugu sehemu ya JNIA – Pugu (km 8.0) kuwa njia sita. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi jumla ya shilingi milioni 242.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi za usanifu.

UPANUZI WA BARABARA YA KIMARA – KIBAHA (KM 25.7) IKIJUMUISHA UPANUZI WA MADARAJA YA KIBAMBA, KILUVYA NA MPIJI – SHILINGI MILIONI 101.000

206. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kupanua barabara ya Kimara – Kibaha ikijumuisha upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji, kuwa njia sita. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya shilingi milioni 101.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza usanifu.

UJENZI WA BARABARA YA KISARAWA – MLANDIZI (KM 52) – SHILINGI MILIONI 162.000

207. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi ni kujenga barabara ya Kisarawe – Mlandizi kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha

2015/16, jumla ya Shilingi milioni 162.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza usanifu.

**UPANUZI WA BARABARA YA BANDARI,
UJENZI WA BARABARA YA DOCKYARD NA
MIVINJENI (KM 2.9) – SHILINGI MILIONI
20.000**

208. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kupanua barabara ya Bandari (km 1.2), ujenzi wa barabara ya Dockyard (km 0.7) na Mivinjeni (km 1.0). Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 20.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu.

**UJENZI WA BARABARA YA PUGU – KIFURU –
MBEZI MWISHO – MPIJI MAGOE – BUNJU
(KM 34) – SHILINGI MILIONI 484.000**

209. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kupanua barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34) kuwa njia tatu. Mradi huu unatekelezwa katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na sehemu ya pili ni Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3). Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 242.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanya mapitio ya

usanifu wa sehemu ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7). Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 242.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza usanifu wa sehemu ya Mbezi Mwisho – Mpiji – Magoe – Bunju (km 21.3).

UJENZI WA MIZANI KARIBU NA BANDARI YA DAR ES SALAAM – SHILINGI MILIONI 41.000

210. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 41.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa mizani hiyo.

BARABARA YA TUNDUMA – SUMBAWANGA (KM 222.8) – SHILINGI MILIONI 2,450.000

211. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Tunduma – Sumbawanga yenye urefu wa kilometa 222.8 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Milenia (Millennium Challenge Corporation - MCC) na mchango wa Serikali ya Tanzania. Utekelezaji wa mradi umegawanywa katika sehemu tano ambazo ni Tunduma – Ikana (km 64) iliyokamilika mwezi Novemba,

2013; Ikana – Laela (km 64) iliyokamilika mwezi Oktoba, 2013; na Laela – Sumbawanga (km 96.5) iliyokamilika mwezi Desemba, 2014; Tunduma – Ikana (Tunduma Township) (km 1.6) iliyokamilika mwezi Februari, 2015; na Tunduma – Ikana (Mpemba – Isongole road) (km 51.20) ambayo usanifu wa kina umekamilika na taaratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

212. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 483.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya mji mdogo wa Tunduma. Aidha, Shilingi milioni 1,967.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.20).

BARABARA YA KAGOMA – LUSAHUNGA (KM 154) – SHILINGI MILIONI 3,890.000

213. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Biharamulo – Lusahunga yenye urefu wa kilometa 294 iliyofanyiwa usanifu mwaka 1996 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Ujenzi wa sehemu ya barabara ya Mutukula – Muhutwe – Kagoma ulikamilika Septemba, 2004 kwa gharama ya Shilingi milioni 17,359.83 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa OPEC.

Aidha, ujenzi wa kiwango cha lami katika sehemu ya barabara ya Kagoma – Lusahunga (km154) ulikamilika Desemba, 2013. Kazi za ujenzi zimegharamiwa na Serikali ya Tanzania.

214. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, barabara ya Kagoma – Lusahunga (km154) imetengewa kiasi cha Shilingi milioni 3,890.000 kwa ajili ya malipo ya mkandarasi.

**BARABARA YA ARUSHA – NAMANGA (KM 105)
– SHILINGI MILIONI 903.000**

215. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya Arusha – Namanga (km 105) – Athi River ni sehemu ya mradi wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaojumuisha nchi za Tanzania na Kenya ambao unafadhiliwa na *Japan Bank for International Cooperation* (JBIC) kwa kushirikiana na Serikali za Tanzania na Kenya. Lengo la mradi ni kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi zimekamilika Desemba, 2012. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 903.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi.

**BARABARA YA SINGIDA – BABATI – MINJINGU
– ARUSHA (KM 321.5) – SHILINGI MILIONI
1,535.340**

216. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Singida – Babati –Minjingu yenye urefu wa kilometa 223 na kukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Minjingu–Arusha yenye urefu wa kilometa 98.

217. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa barabara ya Singida – Babati – Minjingu umegawanywa katika sehemu tatu za Singida – Katesh (km 65.1), Katesh – Dareda (km 73.8) na Dareda – Babati – Minjingu (km 84.6). Ujenzi na ukarabati wa barabara ya Singida – Babati – Minjingu – Arusha (km 321.5) umekamilika. Miradi hii imegharamiwa na ADB, JICA, Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania.

218. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 180.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 1,355.340 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Arusha - Minjingu.

**BARABARA YA DAR ES SALAAM – MBAGALA
(KILWA ROAD) – GEREZANI (SEHEMU YA
KAMATA – BENDERA TATU KM 1.3) –
SHILINGI MILIONI 2,037.702**

219. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kukarabati na kupanua barabara ya lami sehemu ya Gerezani kutoka njia mbili za sasa hadi nne chini ya msaada kutoka Serikali ya Japan na kuchangiwa na Serikali ya Tanzania na usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe. Katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 810.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 985.702 fedha za nje kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi kwa sehemu ya Kamata – Bendera Tatu (km 1.3). Aidha, fedha hizi zinajumuisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina sehemu ya barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe pamoja na daraja la Mzinga ambapo Shilingi milioni 242.000 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

**BARABARA YA MSIMBA – RUAHA/IKOKOTO
MAFINGA – IGAWA (KM 655.3) – SHILINGI
MILIONI 11,893.763**

220. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara ya lami ya Dar es Salaam – Tunduma (TANZAM).

Ukarabati wa sehemu ya Iyovi – Kitonga Gorge (km 86.3), Ikokoto – Iringa (km 60.9) na barabara ya mchepuo kuingia Iringa Mjini (km 2.1) umekamilika Septemba, 2012. Ukarabati wa barabara ya Iringa – Mafinga (km 68.9) umekamilika Agosti, 2013. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha kutoka Serikali ya Denmark pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania.

Aidha, mradi huu unajumuisha ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Mafinga – Igawa (km 137.9) ambapo kazi imeanza kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Vile vile unajumuisha barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152), Njombe – Ndulamo – Makete (km 109), Njombe – Lupembe – Madeke (km 125) na Igawa – Mbarali – Ubaruku (Sehemu ya Mbarali – Ubaruku km 8.9) ambapo maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani yanaendelea.

221. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 701.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa barabara ya Iringa – Mafinga (km 68.9). Jumla ya Shilingi milioni 81.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 7,392.763 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Mafinga – Igawa yenye urefu wa kilometa 137.9. Aidha, Shilingi

milioni 203.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Igawa – Madibira – Mafinga, Shilingi milioni 1,144.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete, Shilingi milioni 1,405.000 kwa ajili ya ujenzi wa Njombe – Lupembe – Madeke na Shilingi milioni 967.000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Igawa – Mbarali – Ubaruku (Sehemu ya Mbarali – Ubaruku km 8.9).

BARABARA YA KOROGWE – MKUMBARA – SAME (KM 172) – SHILINGI MILIONI 8,953.316

222. ***Mheshimiwa Spika***, lego la mradi huu ni kukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara kutoka Korogwe – Mkumbara –Same (km 172). Mradi huu wa ukarabati unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

223. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 82.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 8,871.316 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati wa barabara hii.

BARABARA YA MBEYA – MAKONGOLOSI (KM 115) – SHILINGI MILIONI 5,405.000

224. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mbeya hadi

Makongolosi (km 115) kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (km 36); Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 43). Ujenzi wa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) ulianza Septemba, 2007 na ulitegemewa kukamilika Machi, 2010. Hata hivyo, mkataba wa ujenzi ulisitishwa Aprili, 2009 baada ya Mkandarasi kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba. Mkataba na Mkandarasi mwingine ulisainiwa na kazi za ujenzi zimeanza na zinaendelea. Kwa sehemu ya Lwanjilo – Chunya (km 36) kazi za ujenzi zilikamilika Desemba, 2014.

225. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,645.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo, Shilingi milioni 2,029.000 kwa sehemu ya Lwanjilo – Chunya na Shilingi milioni 606.000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi. Aidha, Shilingi milioni 125.000 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mhandisi Mshauri aliyefanya upembuzi na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa.

**BARABARA YA CHALINZE – SEGERA – TANGA
(KM 244.9) NA MSOGA – MSOLWA (KM 10) –
SHILINGI MILIONI 693.000**

226. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuifanyia ukarabati na upanuzi barabara ya Chalinze – Segera hadi Tanga. Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni: Chalinze – Kitumbi (km 125) na Kitumbi – Segera – Tanga (km 120). Ujenzi wa sehemu ya Chalinze – Kitumbi ulianza Aprili, 2008 na ulikamilika Oktoba, 2010. Mkataba kwa sehemu ya Kitumbi – Segera – Tanga ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010 na umekamilika Februari, 2014. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass) zimekamilika.

227. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 288.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa sehemu ya Kitumbi – Segera – Tanga. Aidha, Shilingi milioni 405.000 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass).

BARABARA YA ITONI – LUDEWA – MANDA (KM 211) – SHILINGI MILIONI 1,783.000

228. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,783.000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu yenye urefu wa kilometa 50 za barabara ya Itoni – Ludewa – Manda.

DARAJA JIPYA LA RUVU CHINI (NEW LOWER RUVU BRIDGE) – SHILINGI MILIONI 284.000

229. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga daraja jipya katika Mto Ruvu kwenye barabara ya Bagamoyo – Msata. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 284.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Ruvu Chini.

BARABARA YA DODOMA – IRINGA (KM 260) – SHILINGI MILIONI 4,234.318

230. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (km 260) pamoja na barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass). Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo

nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Utekelezaji wa mradi umegawanywa katika sehemu tatu za Iringa – Migori (km 95.2), Migori – Fufu Escarpment (km 93.8) na Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.9). Mradi wa Iringa – Migori (km 95.2) unaendelea, ujenzi wa barabara sehemu ya Migori – Fufu Escarpment (km 93.8) umekamilika Januari, 2015 na Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.9) umekamilika Julai, 2014.

231. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 249.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 2,094.616 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Iringa – Migori, Shilingi milioni 218.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 542.136 fedha za nje kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa barabara ya Migori – Fufu Escarpment na Shilingi milioni 237.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 443.566 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa barabara ya Fufu Escarpment – Dodoma. Aidha, Shilingi milioni 450.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Iringa Bypass.

BARABARA YA DODOMA – BABATI (KM 261) – SHILINGI MILIONI 15,722.272

232. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati (km 261). Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela – Bonga (km 88.80) na Bonga – Babati (km 19.2).

Ujenzi wa barabara sehemu ya Dodoma – Mayamaya unaendelea. Ujenzi wa sehemu ya Bonga – Babati (km 19.2) ulikamilika Aprili, 2013. Ujenzi wa sehemu hizi mbili unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Aidha, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mayamaya – Bonga (km 188.15) zinaendelea kwa fedha za mkopo nafuu kutoka AfDB na JICA.

233. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 2,028.000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Dodoma – Mayamaya, na Shilingi milioni 967.000 kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa sehemu

ya Bonga – Babati pamoja na barabara ya mchepuo ya kuingia mjini Kondoa.

234. **Mheshimiwa Spika**, Shilingi milioni 406.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 12,321.272 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mayamaya – Bonga ambayo imegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

(i) Mayamaya – Mela (km 99.35):

Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 203.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 6,160.636 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

(ii) Mela – Bonga (km 88.80):

Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 203.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 6,160.636 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**MASASI- SONGEA – MBAMBA BAY (KM 623.3)
NA MASASI – NEWALA – MTWARA (KM 209) –
SHILINGI MILIONI 34,896.165**

235. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara

ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 623.3). Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika sehemu za Masasi – Mangaka (km 54), Mangaka – Tunduru (km 146), Mangaka –Mtambaswala (km 65.5), Namtumbo – Kilimasera (km 60.7); Kilimasera – Matemanga (km 68.2), Matemanga – Tunduru (km 58.7), Mbinga – Mbamba Bay (km 66) na Masasi – Newala – Mtwara (km 209).

236. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa sehemu ya Masasi – Mangaka umekamilika na umegharamiwa na Serikali za Japan na Tanzania. Kwa sehemu ya Mangaka – Tunduru na Mangaka – Mtambaswala ujenzi kwa kiwango cha lami umeanza na unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (JICA). Kwa barabara ya Tunduru – Matemanga – Songea, sehemu za Namtumbo – Kilimasera (km 60.7); Kilimasera – Matemanga (km 68.2) na Matemanga – Tunduru (km 58.7) ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea chini ya ufadhili wa ADB na JICA. Ujenzi wa sehemu zote tatu kwa kiwango cha lami ulianza tarehe 14 Machi, 2011 lakini kutokana na Mkandarasi kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ilisitisha Mkataba na Mkandarasi.

Hata hivyo, Ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Namtumbo – Kilimasera (km 60.7), Kilimasera – Matemanga (km 68.2) na Matemanga – Tunduru (km 58.7) unaendelea.

237. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa barabara ya Songea – Namtumbo na Peramiho – Mbinga (km 145), ujenzi wa sehemu hizi umegharamiwa kwa fedha za msaada wa kutoka Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa MCC na mchango wa Serikali ya Tanzania na kazi zimekamilika. Aidha, mkataba wa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Masasi – Newala – Mtwara umesainiwa.

238. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, Shilingi milioni 258.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 5,694.844 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mangaka – Nakapanya na Shilingi milioni 244.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 5,377.406 fedha za nje kwa sehemu ya Nakapanya – Tunduru. Shilingi milioni 240.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 5,298.047 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Mangaka – Mtambaswala na Shilingi milioni 216.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 4,782.212 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Tunduru – Matemanga. Kwa

sehemu ya Matemanga – Kilimasera Shilingi milioni 250.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 5,512.317 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Aidha, Shilingi milioni 220.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 4,834.339 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Kilimasera – Namtumbo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa mradi katika kipindi cha uangalizi wa ufanisi wa mradi huu ni Shilingi milioni 7.000 fedha za ndani kwa barabara ya Songea – Namtumbo na Shilingi milioni 7.000 fedha za ndani kwa barabara ya Peramiho – Mbinga.

239. ***Mheshimiwa Spika***, kiasi cha Shilingi milioni 942.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu tayari kwa kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay. Aidha, Shilingi milioni 1,013.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Masasi – Newala – Mtwara.

UJENZI WA MAKAO MAKUU YA WAKALA WA BARABARA – SHILINGI MILIONI 2,157.000

240. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga Makao Makuu ya Wakala wa Barabara pamoja na kuanza ujenzi wa Ofisi za mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu,

Njombe na Lindi. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za ndani. Usanifu wa jengo la Makao Makuu ya Wakala umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 2,157.000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa makao makuu ya Wakala na ofisi za mikoa.

UJENZI WA BARABARA YA KUINGIA UONGOZI INSTITUTE SHILINGI MILIONI 612.796

241. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye Chuo cha Uongozi pamoja na barabara zilizoko ndani ya Chuo hicho. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 612.796 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia Chuo cha Uongozi pamoja na barabara zilizoko ndani ya Chuo hicho.

USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

**Usalama Barabarani – Shilingi Milioni
2,124.000**

242. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu una lengo la kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Katika

mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi milioni 1,624.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 500.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya usalama barabarani kama ifuatavyo:

- i. Mradi wa ujenzi wa mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari yakiwa katika mwendo (Weigh In Motion). Katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha Shilingi 108.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mizani ya kisasa (WIM) eneo la Mikese (Morogoro);
- ii. Ujenzi wa vituo vya pamoja vya ukaguzi (One Stop Inspection Stations) umetengewa shilingi milioni 710.00 fedha za ndani;
- iii. Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani nchini (National Road Safety Authority) umetengewa Shilingi milioni 68.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 250.000 fedha za nje;
- iv. Mapitio ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani zimetengwa Shilingi milioni 58.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 200.00 fedha za nje;

- v. Ukaguzi wa usalama wa barabara (road safety audit) umetengewa Shilingi milioni 82.000 fedha za ndani; na
- vi. Uandaaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani (Road Accident Information System) umetengewa Shilingi milioni 493.000 fedha za ndani na Shilingi milioni 50.000 fedha za nje.

Usalama, Mazingira na Marekebisho ya Mfumo – Shilingi Milioni 226.000

243. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu una lengo la kugharamia shughuli za Usalama na Mazingira pamoja na Marekebisho ya Mfumo wa utekelezaji wa shughuli katika maeneo haya. Katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 226.000 fedha za ndani. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 112.000 zimetengwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Usalama Barabarani kwa shule za kanda ya kati kwa mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora. Kiasi cha Shilingi milioni 81.000 zimetengwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Usalama Barabarani kwa umma (Road Safety Awareness Campaign) kupitia vyombo vya habari. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 33 zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa Idara.

Menejimenti na Utunzaji wa Mazingira – Shilingi Milioni 220.836

244. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu una lengo la kuelimisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika Sekta ya Ujenzi. Vilevile kuandaa program mbalimbali za udhibiti wa uchafuzi wa kimazingira unaosababishwa na shughuli zitokanazo na kazi za ujenzi.

245. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Shilingi milioni 220.836 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya:

- i. Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekta ya Ujenzi;
- ii. Kutoa mafunzo kuhusu tathmini na usimamizi wa mazingira katika Sekta ya Ujenzi kwa wahandisi na mafundi sanifu kutoka TANROADS, TEMESA, TBA na Taasisi zote katika Sekta ya Ujenzi;
- iii. Kutoa mafunzo kuhusu utunzaji na usimamizi wa mazingira katika sekta ya ujenzi kwa Wakurugenzi na Mameneja kutoka TANROADS, TEMESA na TBA;

- iv. Kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (pollution control programme) ikihusisha kuandaa mfumo wa kutunza na kuhifadhi mazingira; na
- v. Kutoa elimu (Awareness campaign) ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira barabarani.

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

246. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi **866,630,000,000.00**. Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa Shilingi **606,640,000,000.00**. Kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kiasi cha Shilingi **259,990,000,000.00** kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2015/16.

247. ***Mheshimiwa Spika***, katika fedha zilizotengwa chini ya Wizara ya Ujenzi ambazo ni Shilingi **606,640,000,000.00**, TANROADS imetengewa Shilingi **541,280,606,000.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi imetengewa Shilingi **60,142,289,600.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa

barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, Shilingi **5,217,104,400.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

248. **Mheshimiwa Spika**, fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi zitatumika kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

- (i) Miradi ya Barabara za Mikoa ambayo imetengewa Shilingi **34,409,894,000.00;**
- (ii) Miradi ya Barabara Kuu ambayo imetengewa Shilingi **15,443,041,000.00;**
- (iii) Miradi ya vivuko imetengewa Shilingi **5,353,899,000.00**. Kati ya fedha hizo Shilingi **1,700,000,000.00** ni kwa ajili ya ununuzi wa Kivuko cha Pangani, Shilingi **2,155,254,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo eneo la Jangwani Beach, Shilingi **1,198,645,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa vivuko na Shilingi **300,000,000.00** ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya vivuko;

(iv) Usimamizi na ufuatiliaji pamoja na kazi zinazohusu shughuli za barabara Shilingi **3,106,262,600.00;**

(v) Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira Shilingi **1,829,193,000.00.**

Mchanganuo wa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi umeonyeshwa katika **Kiambatanisho Na. 3.**

MAELEZO YA MIRADI YA BARABARA INAYOTEKELEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

249. *Mheshimiwa Spika,* fedha zilizotengwa kwa mwaka wa 2015/16 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miradi ya barabara kuu ni Shilingi milioni **15,213.041.** Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo;

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco (km 178) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco (km 124) – Shilingi Milioni 433.00

250. *Mheshimiwa Spika,* lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco yenye urefu wa kilometa 124. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

251. ***Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 433.00 zimetengwa kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bugene–Kasulo/Benaco yenye urefu wa km 124.

Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida km 460 (FS & DD) – Shilingi Milioni 130.00

252. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Handeni – Kiberashi – Kondoa kwa lengo la kujenga kwa kiwango cha lami. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 130.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni.

Barabara za Juu na Malipo ya Fidia TAZARA – Shilingi Milioni 400.00

253. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kulipa fidia kwa mali na kuhamisha miundombinu ya huduma za kijamii zitakazoathirika na ujenzi wa “flyover” katika

eneo la TAZARA. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 400.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuji – Matala – Oldeani Jct (km 328) Shilingi Milioni 1,000.00

254. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Barabara ya Ipole – Rungwa (km 172) – Shilingi Milioni 400.00

255. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya Shilingi milioni 400.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Kuimarisha Uwezo wa Maabara Katika Ufuatiliaji na Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara (Central Materials Laboratory) – Shilingi Milioni 1,000.00

256. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni ununuzi wa vifaa vya Maabara, usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa miradi ya barabara ili kuhakikisha ujenzi huo unakidhi viwango vilivyowekwa. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo (Standards and Specifications) – Shilingi Milioni 300.00

257. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kupitia na kuandaa nyaraka mbalimbali zinazohusu miongozo ya viwango mbalimbali vya usanifu, ujenzi na matengenezo ya miradi ya barabara na madaraja (*standards and specifications*). Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, jumla ya Shilingi milioni 300.00 zimetengwa kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kupitia na kukamilisha mwongozo wa madaraja (*Standard Specifications for Bridge Works*) pamoja na kanuni za Sheria ya Barabara.

Ufuatiliaji na Matengenezo ya Magari kwa Ajili ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo – Shilingi Milioni 1,200.00

258. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni Wizara kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya barabara kuu, madaraja na kuhakikisha ubora unazingatiwa. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya Shilingi milioni 1,200.00 zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya barabara, madaraja, na matengenezo ya magari kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Ujenzi wa Maeneno ya Kupishana Magari Kwenye Milima na Barabara Mbadala ya Kupanda Milima– Shilingi Milioni 150.00

259. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya kupishana magari na barabara mbadala za kupanda milima katika barabara kuu. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya Shilingi milioni 150.00 zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Malipo ya Awali na Fidia kwa Miradi ya Maendeleo – Shilingi Milioni 3,083.041

260. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kulipa malipo ya awali (advance

payments) na kulipa fidia. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 3,083.041 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya awali ya Makandarasi na fidia.

Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92) – Shilingi Milioni 100.00

261. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 100.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50) – Shilingi Milioni 100.00

262. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 100.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Kupunguza Msongamano katika Barabara za Jiji la DSM (Decongestion of DSM Roads) – Shilingi Milioni 2,472.000

263. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara sita za kupunguza msongamano kwenye barabara za katikati ya jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 580.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Goba – Mbezi Mwisho, Shilingi milioni 700.00 barabara ya Tangi Bovu – Goba, Shilingi milioni 265.00 barabara ya Kimara – Baruti – Msewe, Shilingi milioni 345.00 barabara ya Kimara – Kilungule – External (External Maji Chumvi), Shilingi milioni 382.00 kwa barabara ya Kifuru – Kinyerezi na Shilingi milioni 200.00 kwa barabara ya Tabata Dampo – Kigogo.

Daraja la Kigongo/Busisi katika Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 424) – Shilingi Milioni 700.000

264. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kigongo/Busisi. Katika mwaka wa fedha

2015/16, jumla ya Shilingi milioni 700.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 40) – Shilingi Milioni 100.000

265. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga barabara ya Kazilambwa – Chagu kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha wa 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 100.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Barabara ya Urambo – Kaliua (km 33) – Shilingi Milioni 100

266. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga barabara ya Urambo – Kaliua kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha wa 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 100.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 96.7) – Shilingi Milioni 900.000

267. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi kwa kiwango cha lami. Katika mwaka

wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 900.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Barabara Zinazounganisha Bandari Mpya ya Bagamoyo (Km 87.1) – Shilingi Milioni 800.00

268. *Mheshimiwa Spika*, Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazounganisha bandari mpya ya Bagamoyo ambazo ni barabara ya Tegeta – Bagamoyo (km 43.2), Makofia – Mlandizi (km 36.7) na Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, jumla ya Shilingi milioni 800.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Tegeta – Bagamoyo (km 43.2) Shilingi milioni 450.00, Makofia – Mlandizi (km 36.7) Shilingi milioni 250.00 na Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) Shilingi milioni 100.00.

Kuwajengea Uwezo Watumishai wa Sekta ya Ujenzi – Shilingi Milioni 500.00

269. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kujenga uwezo wa ndani wa wataalamu kwenye sekta ya Ujenzi ili kupunguza utegemezi wa wataalamu kutoka nje. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 500.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Barabara ya Mchepuo ya Uyole – Mbalizi – Shilingi Milioni 200.00

270. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanza usanifu wa barabara ya mchepuo kutoka Uyole hadi Mbalizi ili kupunguza msongamano wa magari jijini Mbeya. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 200.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Kuweka Mifumo ya Kompyuta (Software) kwa ajili ya Usanifu wa Barabara na Kuandaa Mipango ya Usafiri (Highway /Transport Planning) – Shilingi Milioni 175.00

271. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi huu ni kuweka mifumo ya kompyuta (software) kwa ajili ya kuandaa mipango ya usafiri na kufanya usanifu wa barabara na kutoa mafunzo kwa wataalam kwa ajili ya utumiaji wa mifumo hiyo. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 175.00 zimetengwa kwa ajili ya kununua mifumo ya kompyuta na kutoa mafunzo kwa wataalam.

**Kupunguza Msongamano – Jiji la Mwanza
(Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha) –
Shilingi Milioni 1,200.00**

272. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kujenga daraja la waenda kwa miguu la furahisha. Kazi za ujenzi wa daraja hili zinagharimiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya Shilingi milioni 1,200.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili.

**Barabara za Mikoa Zitakazotekelezwa kwa
Fedha za Mfuko wa Barabara**

273. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya ukarabati na kuboresha jumla ya kilometa **635.5** kwa kiwango cha changarawe na kilometa **28.7** kiwango cha lami. Kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zitafanyika katika baadhi ya barabara zilizopo Mikoa yote hapa nchini. Aidha, madaraja **20** yatajengwa katika Mikoa mbalimbali nchini na km **833.4** zitafanyiwa upembuzi yakinifu. Kiasi cha Shilingi **34,409,894,000.00** kitatumika kutekeleza miradi hiyo. Orodha ya Miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa

kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4.**

MPANGO WA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2015/16

274. *Mheshimiwa Spika*, fedha za Mfuko wa Barabara zitakazotumika kufanya matengenezo ya Barabara Kuu, Barabara za Mikoa pamoja na madaraja kwa mwaka wa fedha 2015/16 ni jumla Shilingi **541,280,606,000.00**. Mchanganuo wa mpango huo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5A** hadi 5E.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Wakala wa Barabara

275. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wakala wa Barabara (TANROADS) utaendelea kusimamia kazi za kujenga, kukarabati, kujenga na kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa jumla ya **kilometa 35,000**. Matengenezo ya barabara kuu na mikoa yatahusisha matengenezo ya kawaida

(routine maintenance) **kilometa 31,883**, matengenezo ya muda maalum **kilometa 6,096** na **madaraja 3,332**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za utawala na usimamizi wa kazi, udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura, mradi wa matengenezo ya muda mrefu na kazi zinazosimamiwa toka makao makuu za mipango, usalama barabarani na hifadhi ya barabara. Wakala pia utaendelea kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara kuu ambapo **kilometa 523** ni ujenzi mpya kwa kiwango cha lami na **kilometa 113** ni za ukarabati kwa kiwango cha lami na kuendelea na ujenzi wa **madaraja 11**.

276. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo ya barabara za mikoa, Wakala umepanga kujenga **kilometa 77** kwa kiwango cha lami, kukarabati **kilometa 1,252** kwa kiwango cha changarawe na kukarabati **madaraja 30**.

Wakala wa Majengo ya Serikali

277. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wakala utaimarisha utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi za Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Aidha, Wakala utaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea

pamoja na mradi maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi wa Umma. Vile vile, Wakala wa Majengo utaendelea na ujenzi wa nyumba 149 za TAMISEMI pamoja na kuendelea kufanya matengenezo ya nyumba za Serikali ikiwa ni pamoja na kununua samani kwa ajili ya nyumba za Serikali. Kazi zingine zitakazofanywa na Wakala wa Majengo ni kuimarisha Kikosi chake cha Ujenzi kwa kutoa mafunzo na kununua vifaa pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi wake ili kuwaongezea uwezo wa kutumia vifaa vya kisasa katika utendaji wao wa kazi.

Wakala wa Ufundi na Umeme

278. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara kupitia TEMESA imepanga kufanya ununuzi wa vivuko vitakavyofanya kazi kati ya Magogoni – Kigamboni, Kigongo –Busisi na Pangani–Bweni. Aidha, Wakala utakamilisha ukarabati wa vivuko vinne (4) vya MV Nyerere, MV Magogoni, MV Mwanza, na MV Pangani II pamoja na kusimamia ukarabati na matengenezo kwa vivuko na magari ya Serikali.

Wakala pia utaendelea na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo pamoja na maegesho ya vivuko kwa maeneo ya Kirumba, Igogo, Mkuyuni, Butimba, Sweya na Luchebele katika jiji la Mwanza. Aidha, Wakala

utakamilisha ujenzi wa maegesho katika vivuko vya Iramba – Majita, Bukondo – Zumacheli, Ilagala–Kajeje, Msanga Mkuu –Msemo, Kilombero, Bugolola na Kahunda – Maisome.

Wakala pia utafanya upanuzi wa sehemu ya maegesho ya Kigamboni pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria kwa kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo. Kazi nyingine ni kufanya ununuzi wa mashine za kielektroniki za kukatia tiketi (ticket vending machines) kwa ajili ya vivuko vya Kisorya–Rugezi, Ilagala – Kajeje na Pangani–Bweni. Aidha, mfumo wa mashine za kukatia tiketi katika vituo vya Magogoni na Kigamboni utahuishwa.

279. **Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuimarisha karakana kwa kununua vitendea kazi na kufanya ukarabati wa Karakana ya Mt. Depot na Dodoma. Wakala utaendelea kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

Bodi ya Mfuko ya Barabara

280. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi ya Mfuko wa Barabara imepanga kuendelea na jukumu lake la kukusanya fedha na kuzigawa kwa taasisi

zinazofanya kazi za matengenezo ya barabara, ambapo jumla ya Shilingi 866,630,000,000.00 zinatarajiwa kukusanywa. Bodi pia inategemea kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi Dodoma, kununua vifaa 120 vya kupima ubora wa kazi kwa ajili ya Halmashauri zilizobakia na kukamilisha tafiti mbalimbali zinazoendelea na kuwasilisha mapendekezo yanayotokana na tafiti hizo serikalini kwa ajili ya kufikiriwa kutelekeza. Aidha Bodi kwa kushirikiana na EWURA na TRA imepanga kufuatilia mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji mapato kwenye vyanzo vya mapato na kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za mfuko kwa kuendelea na ukaguzi wa kiufundi kwa mikoa yote nchini wakati miradi inaendelea. Bodi imepanga pia kuchapisha nakala za kanuni za matumizi ya fedha za mfuko na kuzigawa katika Halmashauri zote nchini ili zisaidie kuelimisha watendaji na wananchi kwa ujumla.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

281. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi imepanga kusajili Wahandisi 800, Mafundi Sanifu 200 na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 25 pamoja na kusimamia mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi wahitimu 981. Idadi hii inajumuisha wahandisi wahitimu 781 wanaoendelea na mafunzo na 200 ni wapya.

Aidha, Bodi itafanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na Wahandisi waliosajiliwa na kuzingatia maadili ya uhandisi.

Bodi pia itaendelea kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na washauri wote, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla, pamoja na kuwaapisha wahandisi wataalamu na wahandisi washauri wote waliosajiliwa na wanaoendelea kusajiliwa ili kuhakikisha kuwa Wahandisi wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na kuzingatia sheria.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

282. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi inategemea kusajili wataalamu 64, ambapo Wabunifu Majengo ni 31 na Wakadiriaji Majenzi ni 33. Aidha, Kampuni 16 za Wabunifu Majengo na 14 za Wakadiriaji Majenzi zimepangwa kusajiliwa katika kipindi hicho.

Bodi pia itaendelea na mpango wa kuwawezesha wahitimu katika fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi kupata mafunzo kwa vitendo ili kuhakikisha wanapata maarifa na uzoefu unaokidhi haja ya Sekta ya ujenzi kulingana na

sheria. Aidha, Bodi itaendelea kufanya ukaguzi wa miradi iliyopo nchini inayotakiwa kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria sambamba na kuendelea na programu za kutangaza na kuelimisha umma kuhusu shughuli za Bodi na umuhimu wa kushirikisha Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika miradi ya ujenzi.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

283. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi imepanga kusajili jumla ya makandarasi wapya 915 pamoja na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi 2,350. Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi tano za mafunzo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Bodi pia itaendeleza mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na kati (Contractors Assistance Fund – CAF). Jitihada za kuhamasisha makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia zitaendelea, ambapo Bodi imeandaa mkutano wa mafunzo ya utekelezaji miradi kwa ubia kwa makandarasi wa kanda ya kusini utakaofanyika mkoani Mbeya mwezi Septemba, 2015.

Baraza la Taifa la Ujenzi

284. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Baraza limepanga kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria iliyoanzisha Baraza (CAP 162 R.E.2008), kuandaa majarida ya kiufundi kuhusu sekta ya ujenzi, kufanya tafiti mbalimbali za masuala yanayohusiana na sekta pamoja na kuendelea na uboreshaji wa ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi.

Vilevile, Baraza litaendelea na jitihada za kuongeza Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund*), kuratibu mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji (*Construction Sector Transparency Initiative (CoST)*) ikiwa ni njia mojawapo ya kupambana na rushwa katika Sekta pamoja na kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi na utatuzi wa migogoro. Aidha, Baraza litaendelea na ukamilishaji wa jengo la ghorofa 23 la ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na mwekezaji binafsi (Lindi Express Limited).

Vikosi vya Ujenzi

285. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Vikosi vya Ujenzi vitaendelea

na ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za Viongozi wa Serikali, ujenzi wa maegesho ya vivuko (ferry ramps) pamoja na kufanya ukarabati wa ofisi na maghala ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini. Aidha, Vikosi vya Ujenzi vinategemea kuimarisha mradi wa utengenezaji na uuzaji wa vifaa vya ujenzi (Buildings Materials Centre) jijini Dar es Salaam na Dodoma pamoja na kuanza uendelezaji wa viwanja 38 vilivyopo mjini Dodoma.

Vikosi pia vitaendelea na maboresho ya kiutendaji kwa kufanya ukarabati wa karakana za Vikosi vya Ujenzi (Carpentry Workshops) zilizopo Dar es Salaam na Dodoma, ukarabati wa ofisi jijini Dar es Salaam na Arusha pamoja na kuongeza vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

Chuo cha Ujenzi Morogoro

286. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Chuo kinatarajia kufundisha jumla ya wanafunzi **1,390** katika fani za ufundi sanifu na ukaguzi wa barabara, madaraja, majengo, umeme na mitambo pamoja na mafunzo kwa madereva wa Umma (*Public Professional Drivers*), madereva wa awali (*Basic Driving Course*) na madereva wa magari ya abiria (*PSV*).

Chuo kitaendelea na ujenzi wa jengo jipya la maabara ya vifaa vya ujenzi (*materials laboratory*), kuendeleza ujenzi wa karakana ya ufundi, kukarabati majengo 3 na mitambo 3 ya kufundishia na kununua vitendea kazi vya kufundishia.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATTI) - Mbeya

287. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo: Kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe na mafunzo ya uwekaji tabaka la lami kwa kutumia nguvukazi; kuandaa na kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake katika kushiriki kazi za barabara nchini; kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya nguvukazi hapa nchini pamoja na kufanya ziara ya tathmini juu ya mafunzo yaliyotolewa katika mikoa ya Rukwa, Tabora, Singida, Dodoma na Mbeya. Kazi zingine ni pamoja na kuendelea kutoa ushauri na mafunzo maalum kwa viongozi wa vikundi mbalimbali vya ujenzi kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi na

kuelimisha watumishi wa Halmashauri za Wilaya kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia hiyo.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

288. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/16, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na usafirishaji hapa nchini. Kituo kitasambaza majarida yanayohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya ujenzi na usafirishaji pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kimepanga kuendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji hapa nchini. Vilevile, Kituo kitaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Morgan (Morgan State University) cha Marekani na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto za msongamano wa magari katika miji mbali mbali hapa nchini kwa kuanzia na jiji la Dar es Salaam.

MASUALA MTAMBUKA

Maendeleo ya Rasilimali Watu

289. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kuwaendeleza watumishi wake ili kuwaongezea uzoefu wa kikazi na kitaaluma. Watumishi watapandishwa vyeo kwa kuzingatia tararibu na sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na taarifa za Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi (OPRAS). Aidha Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake wa kada mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Habari, Elimu na Mawasiliano

290. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kuujulisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kupitia vipindi vya televisheni, radio, tovuti (www.mow.go.tz) pamoja na machapisho.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

291. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Wizara pia imepanga kutekeleza Mfumo wa kuweka

kumbukumbu za nyaraka taarifa zinazolingia, kutoka au zilizofanyiwa kazi ndani ya Wizara (Document Management System). Wizara itaboresha miundombinu ya mawasiliano inayotumia TEHAMA (Local Area Network) ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia. Mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa watumishi ili kuendana na mabadiliko yatakayojitokeza ya teknolojia hii ya TEHAMA. Wizara pia itaendelea kuwahamasisha wadau wake kutumia TEHAMA katika kupata huduma ili kuwapunguzia usumbufu na kujenga mazingira ya uwazi katika kupata huduma Serikalini.

Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara Nchini

292. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imepanga kuendelelea kuwahamasisha wanawake na jamii kwa ujumla umuhimu wa kushiriki kwa wingi na kikamilifu katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itakamilisha miongozo ya namna ya kufanikisha ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara na kutoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya miongozo hiyo. Wizara pia itaendelea kufuatilia maendeleo ya makandarasi na vikundi vya wanawake waliopatiwa mafunzo ya kutumia teknolojia ya nguvukazi kuanzia mwaka 2010 hadi 2015. Aidha, Wizara itatayarisha mfumo

wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha uratibu na upatikanaji wa taarifa muhimu za makandarasi hao na kuwezesha kusaidia kutatua changamoto wanazopitia katika kazi zao. Wizara kupitia Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara itaendelea kuhamasisha wasichana walio katika shule za sekondari wasome masomo ya sayansi ili kuongeza idadi ya wanawake katika fani ya uhandisi.

Kudhibiti Rushwa

293. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika mwaka wa fedha 2015/16, itaendelea kupambana na rushwa katika sekta ya ujenzi kwa kutoa elimu juu ya athari za kutoa na kupokea rushwa kwa watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha watumishi kutumia dawati la malalamiko la Wizara ili kuweza kutatua kero za rushwa katika sekta ya ujenzi.

Mapitio ya Sera ya Ujenzi

294. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara ya Ujenzi itakamilisha mapitio ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo. Mapitio ya Sera yanafanyika kwa lengo la kuiboresha ili iendane na mabadiliko yanayotokea katika Sekta ya Ujenzi. Sera mpya

itazingatia umuhimu wa kuwapa makandarasi wazalendo uwezo na fursa zaidi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

SHUKURANI

295. **Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti kwa kuiongoza Bunge letu hili kwa weledi mkubwa. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili tukufu na kipekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushauri wao wenye tija katika kuendeleza sekta ya ujenzi.

296. **Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii pia kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu katika kuendeleza Sekta ya Ujenzi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini, Abu Dhabi Fund, Denmark (DANIDA), Marekani (MCC), Uingereza (DFID), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait Fund, OPEC Fund, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC.

297. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mhe. Eng. Gerson H. Lwenge (Mb.), Naibu Waziri; Eng. Mussa I. Iyombe, Katibu Mkuu na Eng. Joseph M. Nyamhanga, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake kwa kujituma katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na taifa.

298. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ujenzi, ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari ambao wametupa ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza Sekta hii. Nitumie fursa hii pia kuishukuru Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

Nawashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wao mkubwa waliutoa kwangu nikiwa mbunge wao. Aidha, napenda pia niishukuru familia yangu kwa kunifariji na kuniombea wakati nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

299. *Mheshimiwa Spika*, hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Ujenzi – (www.mow.go.tz).

MAOMBI YA FEDHA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2015/16

300. *Mheshimiwa Spika*, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza Sekta ya Ujenzi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **932,715,351,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kati ya fedha hizo, Shilingi **42,142,581,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambazo zinajumuisha Shilingi **36,778,993,000.00** za Mishahara ya Watumishi na Shilingi **5,363,588,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shilingi **890,572,770,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **198,360,000,000.00** ni fedha za ndani, Shilingi **606,640,000,000.00** ni za Mfuko wa Barabara na Shilingi **85,572,770,000.00** ni fedha za nje.

**MUHTASARI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA
FEDHA 2015/16**

A. Matumizi ya Kawaida	
MAELEZO	KIASI (SHILINGI)
Mishahara	36,778,993,000.00
Matumizi Mengineyo	5,363,588,000.00
Jumla Fedha za Matumizi ya Kawaida	42,142,581,000.00
B. Fedha za Maendeleo	
Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	198,360,000,000.00
Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	85,572,770,000.00
Fedha za Mfuko wa Barabara	606,640,000,000.00
Jumla Fedha za Maendeleo	890,572,770,000.00
JUMLA YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO	932,715,351,000.00

301. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

